# Nipashe

Jumamosi Oktoba 24, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580378

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba : +255716500500
Barua Pepe: circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020



**IGP SIRRO** awaonya waangalizi uchaguzi

UKURASA 4



**AHUKUMIWA** kunyongwa baada kuua kwa mshale

UKURASA 4



# JPM afichua siri za Gambo

UKURASA 2




## Dk. Shein atangaza neema ya mafuta na gesi

UKURASA 3



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na wananchi kupitia vyombo vya habari Ikulu mjini Unguja jana, kuhusu matokeo ya utafiti wa mafuta na gesi asilia Zanzibar. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play  Download on the App Store


# Lissu asimulia alivyopigwa mabomu mkutanoni Lindi

UKURASA 2


MICHEZO **KAZE: KIKUBWA NI POINTI TATU** UK.24  **MAONI, KATUNI** UK.6

# Uswisi yatoa bilioni 40/- kuboresha sekta afya

**Na Enock Charles**

SERIKALI imepokea msaada wa Sh. bilioni 39.59 kusaidia uboreshaji wa huduma za afya nchini katika mkakati wa kupambana na malaria kutoka Serikali ya Uswisi. Jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, baada ya kupokea msaada huo kutoka Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, alisema kuna mikataba miwili ya upokeaji wa fedha hizo.

Alisema mkataba wa kwanza unagharamia mradi wa uboreshaji wa afya na uimarishaji wa mfumo wa afya huku mkataba wa pili ukigharamia mpango mkakati wa kutokomeza malaria na kwamba msaada huo hauna masharti.

"Hawa ni marafiki zetu wa kweli na tunawashukuru sana kwa msaada huu na ikumbukwe kuwa msaada huu hauna masharti yoyote," alisifu.

Alisema katika uboreshaji wa mfumo wa afya, msaada huo unakusudia kuboresha huduma ya afya kwa kupitia mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa wenye malengo mahususi ikiwamo uanzishwaji wa huduma ya msaada wa kitaalamu chini ya uratibu wa kituo cha kuimarisha mifumo ya afya kilichoko Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Katika mpango wa kutokomeza malaria nchini, James alisema kuna malengo mahususi kama vile kuwezesha mpango wa kudhibiti malaria Tanzania ili kuondoa kabisa vifo vinavyotokana na ugonjwa huo na kupanua wigo wa maeneo yasiyokuwa na malaria hadi nusu ya nchi nzima ifikapo mwaka 2030.

Baada ya kukabidhi mikataba hiyo, Balozi wa Uswisi, Chassot, alisema mikataba hiyo itaimarisha uhusiano wa kitaalamu baina ya nchi hizo.

Alisema tangu mwaka 2001, Uswisi imejihusisha kimkakati katika mapambano dhidi ya malaria kupitia taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

# JPM afichua siri za Gambo

**Na Gwamaka Alipipi,**
ARUSHA

MGOMBEA Urais, Dk. John Magufuli (CCM), amesema alimteua Mrisho Gambo kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ili akamsaidie kuupatia maendeleo mkoa huo na hakuwahi kumtumbua wala kuwa na chuki dhidi yake.

Amesema kuwa kabla ya uongozi wa Gambo, Mkoa wa Arusha ulikuwa nyuma kimaendeleo kutokana na kuongozwa na upinzani, hali iliyomsukuma kutafuta viongozi ndani ya serikali watakaomsaidia kuupatia maendeleo, mmoja wao akiwa Gambo.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini hapa alipowahutubia wananchi na wanachama wa CCM wakati wa mkutano wake wa kampeni.

"Arusha ni mji wa utalii, ndiyo maana nikamleta Gambo, hata alivyokwenda kutekeleza miradi, alikuwa anapambana na mbunge wa hapa (Godbless Lema).

"Ninamshukuru kwa kazi nzuri aliyoifanya, sikumfukuza u-RC (nafasi ya mkuu wa mkoa), isingekuwa vyema uwe RC halafu ugombee ubunge, isingekuwa haki na ndiyo maana viongozi wa serikali wote walioenda kugombea ubunge niliwaondoa.

"Huyu (Gambo) aliniaga, aniambia Arusha inakwenda vibaya, ninaomba nikaikomboe, nikamruhusu. Sasa, ninashangaa watu wanasema kwenye majukwaa wanasema simpendi. Ningekuwa simpendi, ningerudisha jina lake?" Dk. Magufuli alihoji.

Alisema Gambo amekuwa akimsumbua mara nyingi katika kuleta maendeleo mkoani Arusha, akitoa mfano wa mradi wa maji wa Sh. bilioni 520 na wa ujenzi wa barabara ya njia nne.

Alisema: "Nitashangaa wana Arusha mtu aliyewatetea kupata mradi huu mkamnyime kura, ningeweza barabara hii kuipeleka sehemu nyingine. Nimekuwa nikimtuma fanya hivi fanya hivi. Msiweke ukabila haujengi, nimeambiwa kampeni za Arusha zinaanza kuzaa ukabila," alisema.

Dk. Magufuli aliwaahidi wananchi wa Arusha kuja na mkakati wa kuligeuza jiji hilo kuwa Calfonia ya Tanzania, akisema tayari uongozi wake umenunua mashine ya X-RAY katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Pia, alisema kumefanyika ukarabati wa hospitali nne za wilaya za Karatu, Longido, Ngorongoro na Arusha Mjini.

Kwenye sekta ya elimu, alisema Sh. bilioni 120.1 zimetumika katika Mkoa wa Arusha kugharamia elimu bure.

Kuhusu maji, zaidi ya miradi 99 imetekelezwa kwenye vijiji 72 ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 161.86 huku vijiji 257 vikipata huduma ya umeme, 136 vikiwa vimesalia.



Mgombea Urais wa CCM, Dk. John Magufuli, akipongezwa na Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa (katikati) na Katibu Mkuu wa CCM mstaafu Abdulrahman Kinana, baada ya kuhutubia maelfu ya wananchi katika mkutano wa kampeni kwenye uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**


**EAGLE RECOVERIES LIMITED**

**NOTISI/MNADA**

KWA NIABA YA **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED** WA S. L. P. 110183, DAR ES SALAAM.TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA MDAIWA ALIYE TAJWA HAPA CHINI ALIPE DENI LAKE ANALODAIWA KWA MUDA MREFU, ENDAPO ATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA. DHAMANA YAKE ITAUZWA KWA RATIBA IFUATAYO.

| NA. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | SIFA YA DHAMANA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 01 | BUIBUI NETWORK LIMITED/ GLADYS CHARLES LUNGUJA | NYUMBA NZURI ILIYOPO KARAKATA-KIPAWA ILALA DAR ES SALAAM, YENYE LISENI YA MAKAZI NO: 017981 KIWANJA NO: ILA/KPW/KRT15/48 | KUANZIA SAA 5 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana
3. Mnunuzi atakayefika bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mnada
4. Endapo mteja atashindwa kumaliza 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
5. Baada ya kukamilisha malipo yote ni jukumu la mnunuzi kumuhamisha mkazi/wakazi waliopo ndani ya dhamana husika.
6. Gharama za kubadilisha hati miliki (Transfer of ownsership) pamoja na gharama nyingine ni juu ya mnunuzi.Wote mnakaribishwa

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**MKURUGENZI MTENDAJI, EAGLE RECOVERIES LIMITED,
S.L.P 34462, DAR ES SALAAM,
SIMU NA.0714 999 916/ 0755 985 844 /0767 830 535
EMAIL: eaglerecoveries2017@gmail.com**

215958802


# Lissu asimulia alivyopigwa mabomu mkutanoni Lindi

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA Urais, Tundu Lissu (CHADEMA), amesimulia namna mikutano yake ya kampeni ilivyosambaratishwa na polisi mkoani Lindi na kushindwa kuwahutubia wananchi.

Akiwa mkoani Lindi jana, Lissu alishindwa kuwahutubia wananchi baada ya Jeshi la Polisi kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya.

Baada ya tukio, Lissu alidai mtendaji wa kata ndiye aliyeamrisha wananchi waliokuwa wakimsikiliza wapigwe mabomu.

Mtaalamu huyo wa sheria alifafanua kuwa jana alipanga kuwa na mikutano sita lakini sintofahamu ikaibuka na kuharibu ratiba yake.

"Nilitakiwa nianzie Mkuranga Pwani, niende Kibiti, Ikwiriri Rufiji, Somanga Kilwa Kaskazini, Kilwa Kivinje na Lindi.

"Tulitakiwa tukitoka Lindi twende Newala, Masasi na tungemalizia Nachingwea, tumeamkia hapa ili tuanze safari, mengine yakaanza. "(Rubani) aliyekuwa anarusha ndege kaiwasha, wakati tunataka tuondoke, mara kaambiwa zima, njoo ofisini kuna habari," Lissu alidai. Mgombea huyo alisema baada ya rubani wao kuitwa na polisi, waliambiwa hawawezi kwenda Nachingwea wala Nanyumbu kwa sababu kuna kimbunga. "Nikiwa bado kwenye ndege nikisubiri, rubani alielezwa kuwa kimbunga kimefika hadi Masasi, hivyo mkutano ufanyike maeneo matatu ikiwamo Lindi.

"Tuliondoka kuelekea Somanga, tukakuta wananchi wameandaa muziki mkubwa, tukakuta askari, alikuja Mtendaji wa Kata na akataka tuonyeshe kibali cha kufanya mkutano Somanga," alisimulia.

Lissu alisema walimjulisha kuwa ratiba ya kampeni inasimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) yenye makao makuu Dodoma siyo na Mtendaji wa Kata, Mkurugenzi wa Wilaya ya Kilwa, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Mkuu wa Mkoa, Waziri Mkuu au Rais. Lissu alisema: "Yule kijana yaelekea alikuwa na nguvu, akawaamuru polisi 'hakuna kufanyika mkutano hapa', tukanyeshewa mvua ya mabomu, nikiwa jukwaani nazungumza, watu wamepigwa mabomu na polisi kwa amri ya mtendaji wa kata," Lissu alilalamika.

Alisema nchi zinazojali demokrasia, wakati wa uchaguzi huwa ni kipindi cha mazungumzo, mikutano na uhuru wa watu kujadiliana kuhusu nchi wanayotaka kuijenga na viongozi wanaotaka kuwa nao.

# Twiga yaonyesha ubia wa kiuhalisia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI madini ya Twiga (TMC) imeonyesha uwezo wa kuongeza thamani na ubia wa kweli kati yake na serikali, ikiwa ni mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwake.

Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni uchimbaji dhahabu ya Barrick, Mark Bristow, alisema hayo jana katika mkutano na waandishi wa habari na ziara ya nne ya kutembelea mgodi.

Twiga ni kampuni ya ubia kati ya kampuni ya Barrick na serikali ya Tanzania na ina jukumu la kusimamia mali za Barrick nchini pamoja na utekelezaji wa makubaliano ya pamoja katika mgawanyo sawa wa kiuchumi baina ya pande husika. Ilianzishwa kuchukua uendeshaji wa iliyokuwa kampuni ya Acacia Mining Septemba, mwaka jana na kuingia mkataba na serikali.

Katika makubaliano hayo, Barrick itailipa serikali Dola za Kimarekani milioni 300 kumaliza mgogoro uliokuwapo na Acacia. Mbali na malipo ya dola milioni 100 kwa ajili ya utatuzi wa mgogoro, Barrick kupitia mali zake nchini, imeilipa serikali zaidi ya dola milioni 200 kwa ajili ya kodi na mirabaha na wiki iliyopita, Twiga ilitangaza kutoa gawio la dola milioni 250.

"Kwa thamani hiyo iliyotolewa katika kipindi kifupi, ni ishara kwamba na ninaamini hiyo ni ubia wa kwanza na wa aina yake kwa Afrika. Katika makubaliano yaliyofikiwa na hayajatekelezwa kwa nguvu zote, tumemaliza migogoro yote na mmiliki wa ardhi na tunaheshimu vibali kuhusu mazingira na sheria za nchi," alisema Bristow.

"Mgodi wa North Mara uliokarabatiwa na kuongezewa uwezo, ni mpango wetu ambao umekuwa katika mpango hadi sasa na Bulyanhulu umeshaanza shughuli za uchimbaji na unatarajiwa kuanza rasmi wa madini mwishoni mwa mwaka huu," alisema.

Barrick imepewa leseni mpya 10 kwa ajili ya utafutaji na uchimbaji na inapanga kutumia dola milioni nane kwa mwaka huu. Kampuni hiyo pia imejikita kushirikiana na wadau zikiwamo jamii zilizoko katika maeneo ya mgodi na kamati ya maendeleo ya jamii iliyoanzishwa North Mara.

Kuhusu usimamizi mazingira, mpango kabambe wa usimamizi wa maji imeanza kutekelezwa. Tangu kuanza kwa shughuli mwaka jana, asilimia 50 ya tatizo la maji machafu lililokuwapo North Mara limeshatatuliwa mpaka sasa.

# Shein atangaza neema ya uwapo mafuta, gesi asilia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema matokeo ya usafirishaji wa taarifa zilizokusanywa kuhusu utafiti wa mafuta na gesi asilia Zanzibar, yameonesha uwapo kwa rasilimali hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari Ikulu mjini Zanzibar jana, Dk. Shein alisema kwa upande wa Unguja, taarifa za mistari zimekuwa na ubora unaoridhisha na kuonyesha maeneo ya miamba yenye maumbile yanayoweza kuhifadhi mafuta na gesi asilia.

Kwa upande wa Pemba, alisema kuna taarifa zinazoonyesha kiwango kidogo cha ubora kutokana na maumbile ya kijiografia ya kisiwa hicho.

Dk Shein alisema serikali inalenga kuhakikisha faida zitokanazo na rasilimali ya mafuta na gesi asilia zinachangia katika ukuaji wa uchumi na kuwanufaisha wananchi bila ubaguzi.

Alisema utafutaji wa mafuta na gesi asilia ni jambo linalohusu maendeleo ya Zanzibar, hivyo kamwe halitakiwi kuleta mifarakano bali liwaunganishe.

Kutokana na hali hiyo, alisema wananchi wanapaswa kujiepusha na baadhi ya watu walioamua kuitumia ajenda hiyo kwa dhamira ya kuwagawa jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya serikali.

Alisema suala la mafuta na gesi asilia ni sehemu ya uchumi wa bluu, jambo ambalo limekuwa likitekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015-2020.

Pia alisema katika ushughulikia wa suala hilo, serikali imeanzisha Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa shughuli za utafutaji, uchimbaji na uendelezaji wa rasilimali hizo.

Alisema katika ushughulikiaji wa suala hilo, serikali ilitia saini mkataba wa mgawanyo wa uzalishaji wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia na kampuni ya RAK Gas kutoka Ras el Khaimah, katika sherehe zilizofanyiika Ikulu Oktoba 23, 2018.

Akizungumzia utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Pemba - Zanzibar chenye ukubwa kilomita za mraba 11,068, Dk. Shein alisema ilianza mwaka 2017 kabla ya kutiliana saini mkataba wa PSA kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya RAK Gas.

"Kazi hiyo ilifanywa ili kuangalia uwezekano wa kuwepo kwa miamba yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta na gesi asilia", alisema.

Kutokana na matokeo yaliyopatikana, alisema ulifanyika uchunguzi kwa njia ya mtetemeko (2 DSeismic Survey) kupitia kampuni ya BGP ya Jamhuri ya Watu wa China katika maeneo ya baharini, nchi kavu na maeneo ya kina kifupi cha bahari.

Alisema kutokana na matokeo hayo, kampuni ya RAK Gas ilichukua hatua ya kuendeleza kazi za utafutaji wa taarifa za mitetemo za mafuta na gesi asilia kwa kitalu cha Pemba-Zanzibar, matokeo yaliyoifanya kuendeleza uchunguzi kwa njia hiyo ya mitetemo katika kina kifupi cha maji, eneo ambalo lilionesha kuwepo viashiria vya gesi asilia.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James na Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Didier Chassot, wakibadilishana mikataba miwili ya msaada wa Faranga za Uswisi milioni 15.75 sawa na Sh. bilioni 39.59 kwa ajili ya uboreshaji na uimarishaji wa mfumo wa afya na utekelezaji wa Programu ya Kutokomeza Malaria Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WFM**

# Vigogo NSSF waachiwa huru uhujumu

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), amewafutia mashtaka watumishi saba kati ya tisa wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka matano, likiwamo la utakatishaji wa zaidi ya Sh. Bilioni mbili.

Aidha, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ilikubali hati ya kuwaondolea mashtaka iliyowasilishwa na DPP na Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Godfrey Isaya kuwaachia washtakiwa hao.

Juzi, DPP aliwasilisha hati akidai kuwa hana nia ya kuendelea na mashtaka dhidi yao, aliomba mahakama iwaachie huru.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Mkuu, Materus Malandu, aliwataja washitakiwa walioachiwa kuwa ni James Oigo, Hellen Peter, Yvonne Kimaro, Restiana Lukwalo, Jamila Vulu, Tikyeba Alphonce na Dominic Mbwete.

Washtakiwa waliobaki katika kesi hiyo ni Mwandishi wa Hundi Abdulrahaman Njozi na Meneja Uhakiki Amiri Kapera, ambao walirudishwa mahabusu. Kesi hiyo iliahirishwa mpaka Novemba 3, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

Katika kesi hiyo, washitakiwa hao wanadaiwa kutenda makosa hayo katika tarehe zisizofahamika kati ya Julai Mosi, 2016 hadi Septemba 4, 2017 jijini Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa katika kipindi hicho washtakiwa hao wakiwa waajiriwa wa NSSF, wakiwa na watu wengine ambao hawako mahakamani, walikula njama ya kutenda kosa la kughushi na utakatishaji fedha.

Ilidaiwa kuwa Njozi na Kapera wakiwa katika ofisi za makao makuu ya NSSF, walighushi hundi 47 za benki ya CRDB za akaunti ya shirika hilo zenye thamani ya Sh. 2,130,211,437.35 kwa lengo la kuonyesha kuwa hundi hizo ni halali zimetolewa na bodi ya wadhamini ya NSSF wakati wakijua si kweli.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao pia katika kipindi hicho, waliiba kiasi hicho cha fedha mali ya bodi ya wadhamini ya NSSF na kuisababishia hasara ya kiasi hicho cha fedha kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Katika shtaka la utakatishaji, washtakiwa hao wanadaiwa kutakatisha Sh 2,130,211,437.35 kwa kujihusisha katika miamala ya fedha hizo wakati wakijua ni zao la makosa tangulizi ya kughushi na wizi.

# Ahukumiwa kunyongwa baada kuua kwa mshale

**Na Samson Chacha,** TARIME

GHATI Gibiti, mkazi wa Kijiji cha Mbirikiri, Tarafa ya Ingwe, wilayani Tarime, mkoani Mara, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya kumuua kwa kukusudia kwa kumchoma mshale wenye sumu Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbirikiri, Mwita Mirumbe.

Mahakama imejiridhisha kuwa Gibiti alimuua Mirumbe wakati kiongozi huyo alipokuwa anatekeleza majukumu yake ya kazi.

Katika kesi hiyo namba 59 ya mwaka 2019 ambayo hukumu yake ilisomwa juzi na Jaji John Kayoza wa Mahakama Kuu ya Musoma wilayani Tarime, Upande wa Mashitaka ulipeleka mashahidi watatu huku Upande wa Utetezi haukuwa na shahidi mwingine zaidi ya mshitakiwa.

Wakili wa Serikali, Jesse Temba, alidai mtuhumiwa Gibiti alifanya mauaji hayo Machi 15, 2017 jioni wakati Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbirikiri (Mirumbe) alipokuwa na walinzi wake walipokwenda kumpelekea barua ya wito mahakamani baada ya kumdhamini ndugu yake aliyekuwa na kesi ya kupatikana na nyara za serikali na kisha mtuhumiwa kutoroka.

Alidai kuwa mwenyekiti huyo na walinzi wake waliondoka na punda wa mshitakiwa ili amfuate punda huyo huko ofisini, lakini wakati wakielekea ofisini kwa mwenyekiti huyo, ghafla Gibiti alijitokeza akiwa na upinde na mishale na kuanza kuwashambulia kwa kuwarushia mishale yenye sumu mara tatu na mshale uliokuwa na sumu ulimchoma kwenye paja la mguu na kusababisha kifo chake.

Katika kesi hiyo, Upande wa Mashataka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Temba, ulileta mashahidi watatu vikiwamo vielelezo vya fomu ya daktari, PF 3 na walinzi waliokuwa na mwenyekiti huyo.

Wakili Temba aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshitakiwa kwa madai kuwa kitendo alichokifanya cha kumuua mwenyekiti ambaye alikuwa kiongozi wa jamii, ni cha kinyama.

Jaji Kayoza wakati wa kutoa hukumu alisema: "Kulingana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapa, bila kuacha shaka yoyote, ninamtia hatiani mtuhumiwa Chacha Ghati Gibiti kwa kosa la kuua kwa kukusudia na kuhukumu kunyongwa hadi kufa ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaokatisha maisha ya wenzao kwa makusudi," alisema Jaji Kayoza.

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshitakiwa alionekana kutokwa machozi huku ndugu wa marehemu Mirumbe waliokuwa nje ya mahakama hiyo wakidai haki imetendeka na wengine kusikika wakisema "mshahara wa dhambi ni umauti".

# IGP Sirro awaonya waangalizi uchaguzi

**Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, amewahakikishia watazamaji wa nje wa uchaguzi mkuu kuwa Tanzania ni salama na jeshi hilo limejipanga vizuri.

Vilevile, IGP Sirro amewaonya watazamaji wa uchaguzi wa ndani na nje ya nchi kuhakikisha hawajiingizi katika uhalifu wa aina yoyote kwa sababu kwa kufanya hivyo, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa watazamaji wa ndani na nje ya nchi ulioandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa lengo la kuwapa taarifa mbalimbali zinazohusu kuelekea uchaguzi mkuu.

IGP Sirro alisema wanapokuwa watazamaji wa uchaguzi, wajue kuwa hawapo juu ya sheria na watakapozivunja, watashtakiwa kama wahalifu wengine.

"Unaweza kutoka nchi uliyotoka, ukifika humu usipofuata katiba na sheria zilizopo, unaweza kujikuta umekuwa mhalifu, ukiwa mhalifu sheria zitachukua mkondo wake, watazamaji wa uchaguzi mjitahidi msivunje sheria," alionya.

Pia, aliwakumbusha watazamaji hao kuwa wamepewa nafasi hiyo, hivyo watende na washauri mambo ya haki pasi na kujiingiza kwenye ushabiki na kujikuta wanakuwa wahalifu.

Mjumbe wa NEC, Balozi Omar Mapuri, alisema tume imetoa idhini kwa taasisi za kimataifa 17 kuwa watazamaji wa uchaguzi mkuu na za ndani ni 97 huku wakalimani wa lugha wakiwa ni 28.

Balozi Mapuri aliwataka watazamaji wa uchaguzi wazingatie miongozo inayowaongoza kufanya utazamaji na wahakikishe hawaingilii kwa namna yoyote mwenendo wa mchakato huo na kusababisha vurugu kutokea.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa NEC, Emmanuel Kavishe, aliwakumbusha watazamaji wa ndani wa uchaguzi kuwa sheria haiwatambui kupiga kura katika kituo ambacho hawajajiandikisha.

Alisema wamekutana na kundi hilo ili kuwaeleza matayarisho ambayo tayari yameshafanyika na yanayoendelea kufanyika.

"Watazamaji wenyewe kwa wenyewe wamesisitizana kuheshimu sheria na kuzingatia miongozo tumewapatia ili uchaguzi uwe wa amani," alisema.

# China yatoa mamilioni kukabili moto Kilimanjaro

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI ya China imeipatia Tanzania Sh. milioni 150 kwa ajili ya kuongeza nguvu katika harakatiza uzimaji wa moto katika Mlima Kilimanjaro.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi fedha hizo jana jijini Dar es Salaam, Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema wameamua kutoa msaada huo kwa kuzingatia uhusiano mzuri uliopo baina ya China na Tanzania.

Alisema Mlima Kilimanjaro ni mlima mrefu na maarufu barani Afrika na duniani kwa ujumla, hivyo hawana budi kusaidiana na serikali kuhakikisha wanamaliza tatizo hilo.

"Sisi Serikali ya China mara nyingi tumekuwa mstari wa mbele pale Tanzania inapopata matatizo, siku chache zilizopita tulikuwa mstari wa mbele lilipotokea tetemeko la ardhi Kagera kwa kusaidia vitu vile vifaa tiba na fedha kwa waathirika.

"Vilevile, kipindi cha corona tulikuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tunatoa mchango ambao utaisaidia serikali katika kujikwamua kutoka kwenye janga hilo," alisema.




Balozi wa China nchini Tanzania Wang Ke (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. million 150 kwa Kamishina Mwandamizi wa Uhifadhi Kaskazini wa Hifadhi za Taifa (TANAPA), Batiho Herman, kwa ajili ya kuongeza nguvu katika uzimaji wa moto unaondelea kuwaka kwenye Mlima Kilimanjaro.

Balozi huyo alisema wameona moto kwenye Mlima Kilimanjaro ulioanza Oktoba 11 na ukaendelea kusumbua kwa muda mrefu, hivyo kuna haja kutoa fedha ili kuongeza nguvu hususani katika kununua vifaa vya kuzimia moto na kurekebishia miundombinu iliyoharibika katika njia za watalii kupanda mlima huo.

Kamishina Mwandamizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kanda ya Kaskazini Tanapa, Batiho Herman, aliishukuru Serikali ya China kwa kuwasaidia kiasi hicho cha fedha.

Alisema msaada huo utawaongeza nguvu kwa asilimia kubwa kukabiliana na matukio ya moto.

"Hizi pesa Sh. milioni 150 tulizozipata leo (jana) ni jambo la kushukuru sana, tena sana kwa Serikali ya China, tutanunua vifaa vya kuzimia moto na tutaweka watu wakae kama walinzi katika mlima huo ili iwe rahisi hata likitokea janga la moto waweze kuzima kiurahisi.

"Lakini pia hata kama vifaa vya kuzimia moto vikibakia mara baada ya zoezi hilo kukamilika, vitahifadhiwa kwa ajili ya tahadhari ya siku nyingine," alisema Kamishina huyo.

Aliongeza kuwa licha ya moto huo kuathiri baadhi ya sehemu za Mlima Kilimanjaro, sekta ya utalii haijaathirika na watalii wanaendelea kuupanda.

"Eneo ambalo limeathirika kwa zaidi ni kilomita za mraba 95.5, kuathiriwa huko ni sawa na tano tu ya eneo lote, kwa hiyo vitu ambavyo vimeathirika pale zaidi ni wadudu wanaotambaa kama nyoka na makinda ya ndege pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kiasi na ni upande wa Malangu ulioguswa," alibainisha.

# DDP: Wananchi mtapata haki

**Na Mwandishi Wetu,**
MUFINDI

MKURUGENZI wa Mashtaka, Biswalo Mganga, amewahakikishia wananchi wa Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa upatikanaji wa haki baina yao bila uonevu wowote.

Wakati wa uzinduzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wilayani hapa juzi, Mganga aliahidi suala hilo akisema kuanzishwa kwa ofisi hiyo wilayani hapa kumelenga kusogeza huduma karibu kwa wananchi walio wengi.

Mganga aliongeza kuwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi ni kuwa na utawala bora, kulinda haki na amani kwa kila Mtanzania na kupunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa na wananchi na kuahidi kuwashughulikia wale wote ambao wanavuruga usalama wa nchi yetu. Mkuu wa Wilaya ya Mufindi alipongeza jitihada hizo za kuhakikisha ofisi hiyo inafunguliwa wilayani hapa, akisisitiza kuwa kufunguliwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kumekuwa faraja kubwa kwa wananchi. Jamhuri William, alisema anaamini wananchi wake watapata elimu ya kutosha juu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka namna inavyofanya kazi na kuhakikisha haki inatendeka baina ya wananchi.

Aliwataka wananchi wake kuitumia vizuri ofisi hiyo na kuhakikisha kutoa ushirikiano ipasavyo.

Wananchi waliohudhuria hafla hiyo waliishukuru Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kuwasogezea wananchi huduma hiyo kwa ukaribu zaidi na kuahidi kuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia wananchi kwa kuwa walikuwa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Edson Makallo, alitoa wito kwa wakuu wa wilaya kuendelea kujitolea ofisi kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa mashtaka kwa kuwa ofisi zilizopo ni chache.

"Hadi sasa, tumefanikiwa kufungua jumla ya ofisi za wilaya 15, ukizingatia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka zinapaswa kuenea jumla ya wilaya 139," alibainisha.




Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Hazina ya jijini Dar es Salaam, Omari Juma (kushoto), akimkabidhi zawadi mwanafunzi aliyemaliza darasa la saba katika shule hiyo, Harris Edward, aliyeshika nafasi ya kwanza kwenye usaili wa kujiunga na shule ya Feza Boys ya jijini humo jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wasomi wanusa harufu siasa chafu

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

WASOMI na wanataaluma mbalimbali mkoani Mbeya wamezungumzia kuhusu kile wanachokiita siasa chafu katika kuwapata viongozi wa kuchaguliwa na wananchi.

Katika Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere lililofanyika Kituo cha Mkoa wa Mbeya cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT) na kuhudhuriwa na washiriki kutoka taasisi za elimu ya juu, wasomi hao waliibua jambo hilo.

Walisema kumeibuka wanasiasa ambao ukikaribia uchaguzi, wanakwenda kwenye majimbo na kuanza kutoa misaada ya kijamii, ikiwa ni mbinu ya kuwashawishi wananchi kuwachagua utakapowadia wakati wa uchaguzi.

Akiwasilisha mada katika kongamano hilo, Mwanafunzi wa CKHT, Heri Hemahema, alisema kumezuka aina hiyo ya siasa ambayo imekuwa ni ya wanasiasa kuanzisha huduma na kutoa misaada muda mfupi kabla ya uchaguzi na hatimaye kugombea, kitu ambacho alisisitiza ni kinyume cha falsafa ya Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema wakati wa kampeni na uchaguzi, wananchi wanapata wakati mgumu kumchagua kiongozi wa aina hiyo kwa sababu ni vigumu kujua nia halisi ya kiongozi huyo.

"Mtu anaanza kutoa msaada wa bati, ukarabati wa miundombinu au utoaji wa huduma miaka au miezi michache kabla ya Uchaguzi na baadaye anapitishwa na chama kuwania nafasi ya uongozi. Hii ni sawa kweli?" Hemahema alihoji.

Mhadhiri na Mkurugenzi wa Kituo cha Mbeya cha CKHT, Maulana Ali, alisema umefika wakati ambapo wananchi wanachanganywa na propaganda za wanasiasa ambazo zinazungumzia maendeleo kwa mtazamo wa vitu badala ya uhalisia wa maisha kwa ujumla.

Alibainisha madhumuni ya kongamano hilo kuwa ni kuwakutanisha wanaataaluma na wasio wanataaluma ili kujadili masuala mbalimbali kuhusu Mwalimu Julius Nyerere ambaye ni Baba wa Taifa na mchango wake kwa taifa katika sekta mbalimbali.

Mhadhiri na Wakili kutoka CKHT Songwe, Scholastica Makoye, alisema bado kuna umuhimu wa mifumo ya kisiasa na kiutawala kuwa huru na kuruhusu mwananchi kutoa maoni yake kwa viongozi hata pale ambapo wameteleza ili kuweka dhana ya uwajibikaji.

"Yapo maeneo machache ambayo viongozi wapo tayari kusikiliza maoni ya watu, kitu ambacho ni kinyume cha falsafa ya Mwalimu Nyerere," alisema Wakili Makoye.

Kongamano hilo lilikuwa na dhima ya kumbukizi ya kujadili mchango wa Mwalimu Julius Nyerere katika nyanja mbalimbali ikiwamo siasa, utamaduni na uchumi hususani katika mwaka huu wa uchaguzi mkuu.

# RC aonya vijana vurugu uchaguzi

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, amewaonya vijana 150 wanaodaiwa kuandaliwa na baadhi ya vyama kufanya fujo kwenye vituo vya kupigia kura Jumatano ijayo wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

Albert Chalamila alitoa onyo hilo jana wakati kikao chake na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu hali ya ulinzi na usalama kuelekea uchaguzi huo.

Alisema wanazo taarifa za makundi hayo kupanga njama za kufanya maandamano, kufunga barabara na kuwafanyia vurugu wasimamizi wa uchaguzi kwenye vituo.

Alisema tayari serikali imepata taarifa kuna vikundi mbalimbali vya vijana ambao wanadaiwa kuandaliwa na vyama vya upinzani kuharibu uchaguzi ikiwa ni pamoja na kufunga barabara, kufanya maandamano na kuwafanyia vurugu wasimamizi wa uchaguzi.

"Tunazo taarifa kwamba kuna makundi yamepanga njama za kuvuruga uchaguzi ikiwamo maandamano, kufunga barabara na kuwafanyia vurugu wasimamizi wa uchaguzi, ninawaonya msitishe zoezi hilo," alisema.

Aliyatajaa baadhi ya majimbo ambayo viongozi wa vyama wanadaiwa kujipanga na kushawishi wananchi kufanya vurugu kuwa ni Rungwe na Mbeya Mjini, akisema serikali halitalifumbia macho suala hilo na tayari imejipanga kukabiliana navyo na haitakubali kuona mtu anapoteza maisha au kupata ulemavu kwenye uchaguzi huo.

Kiongozi huyo wa mkoa pia aliwahamasisha wananchi kujitokeza kwenye vituo vya kupigia kura Oktoba 28 na baada ya kupiga kura, warudi nyumbani kuendelea na majukumu mengine na kutokubali kubaki vituo kwa madai ya kulinda kura kwa kuwa hilo siyo jukumu lao.

Chalamila pia alizungumzia wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuandamana hadi ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mbeya Mjini wakilalamika majina 16 ya wagombea wa chama hicho kuenguliwa kwenye mchakato ya kugombea nafasi ya udiwani na kutoapishwa kwa mawakala wao.

Alisema wafuasi hao walifika kwenye ofisi hiyo na kuanga vilio huku wengine wakijaribu kuvua nguo zao, hali iliyozua taharuki kwa wananchi na viongozi.

Alisema viongozi walitumia busara kwa kuwaacha kuendelea kufanya mambo yao licha ya kuwa alitoa muda wa saa kadhaa wawe wametawanyika eneo hilo.

Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Jimbo hilo, Mwajabu Abdallah, alisema serikali imechukua tahadhari zote za kukabiliana na ugonjwa wa corona kwa kuhakikisha kila Kituo kinaweka ndoo za maji na sabuni ili watu kunawa mikono.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, akawaomba Watanzania kuendelea kuliombea taifa ili uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu.

**■Imeandikwa na Grace Mwakalinga na Nebart Msokwa (MBEYA)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ligi Kuu itumike vizuri kusuka kikosi cha CHAN

**WAKATI** Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 ambayo inashirikisha timu 18 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini iko katika raundi ya saba, hiyo ndio sehemu inayotarajiwa kuandaa wachezaji watakaoitwa kwenye kikosi kitakachoshiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Fainali zijazo za CHAN zitafanyika kuanzia Januari mwakani nchini Cameroon na Tanzania (Taifa Stars), imepangwa katika Kundi D ikiwa pamoja na Zambia, Namibia na Guinea.

Katika fainali hizo, Stars ambayo iko chini ya Kocha Mkuu Mrundi Etienne Ndayiragije, itaanza kampeni za kuwania kombe hilo Januari 19, mwakani kwa kuwavaa Zambia halafu Januari 23 itakutana na Namibia na itamaliza mechi za hatua ya makundi kwa kupambana na Guinea.

Hii ni mara ya pili kwa Taifa Stars kushiriki fainali hizi, mara ya kwanza ilipata tiketi ya kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo mwaka 2008, ikiwa chini ya Mbrazil, Marcio Maximo. Ilikuwa ni michuano ya kwanza kufanyika na ilichezwa nchini Ivory Coast, hata hivyo Stars haikufanya vyema, ilitolewa kwenye hatua za makundi.

Ili Stars iende katika mashindano hayo mwakani ikiwa imara, ni vyema Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), makocha wanaofundisha timu za Ligi Kuu Bara (hasa makocha wazawa) na wasimamizi wote wa michezo ya ligi hiyo wakaitumia vizuri kuwaandaa wachezaji.

Tunaamini na inafahamika kuwa ligi hiyo ndiyo itakayotoa zaidi ya asilimia 98 ya kikosi kitakachokwenda kushiriki fainali hizo, hivyo wachezaji wanatakiwa kusimamiwa vyema kuanzia kwenye mafunzo hadi wanapokuwa uwanjani.

Makocha wanatakiwa kuwaandaa wachezaji hao kupambana, kufahamu sheria na kucheza mchezo wa kiungwana ili kuwaweka tayari na soka la ushindani la kimataifa ambalo watakakutana nalo kwenye fainali za CHAN.

Kama mchezaji atakayeitwa kwenye kikosi cha CHAN hatakuwa na misingi mizuri ya uchezaji, basi itampa wakati mgumu Ndayiragije kwa sababu muda atakaokuwa naye ni mchache kutokana na ratiba.

Pia waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara mnakumbusha kuchezesha kwa kufuata sheria 17 za soka bila ya kupendelea mchezaji wa timu yoyote.

Gazeti hili linaamini waamuzi kwa kufanya hivyo, watakuwa wanawajenga wachezaji wenye uwezo wa kupambana na si kusubiri 'mbeleko', lakini kuwaandaa wachezaji wenye nidhamu wakati wote wa mchezo. Kama mchezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara (hasa Mtanzania), atakuwa anafanya makosa yanayostahili kuadhibiwa na mwamuzi akaacha kutoa adhabu, hapo itakuwa mchezaji huyo hajengwi na badala yake ataona kile alichokifanya ni halali na kitaigharimu nchi pale watakapokuwa kwenye michuano ya kimataifa.

Waamuzi huu ni wakati wenu kuwaandaa wachezaji kwa kufanya maamuzi sahihi na ambayo hayataigharimu nchi, pale nyota watakaoitwa kwenye kikosi cha Stars watakapokuwa kwenye michuano ya kimataifa.

Wachezaji pia wanatakiwa kufahamu vyema majukumu yao na kuhakikisha wanacheza kwa kufuata maelekezo na si kucheza na 'akili' za mashabiki.


Hata hivyo, ushindani unaoonyeshwa na timu zinazoitwa ndogo, unaonekana kuwasumbua vigogo, wa soka nchini, Simba na Yanga, ambao msimu huu wamekuwa wakipata 'tabu' wanapoingia uwanjani kucheza mechi zao na wameacha tabia ya kuingia na matokeo 'mfukoni'. Nipashe inaamini ushindani huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuifanya Stars kuwa imara kwa sababu fainali za CHAN zinashirikisha wachezaji wanaocheza ligi za nyumbani tu.

Fainali hizo ni fursa nyingine kwa wachezaji kwenda kutangaza vipaji vyao na hatimaye kusajiliwa na timu za nje kwa sababu kwenye soka hakuna miujiza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ukimpa mtu kazi ...

Na Barnabas Maro

**"UKIMPA** mtu kazi pataneni ujira kwanza" maana yake unapompatia mtu kazi fulani ya kuifanya lazima kwanza mpatane malipo.

Methali hii yaweza kutumiwa kutukumbusha kwamba tunapaswa kuyazingatia mambo katika upana wake. Mathalani, kabla hatujafanya jambo lolote lazima tuyafikirie matokeo yake. 'Mkataba' ni makubaliano yanayofanywa kwa maandishi baina ya watu, nchi au kampuni mbili ama zaidi kwa ajili ya jambo fulani. Kwa hili ninalojadili, ni makubaliano rasmi ya maandishi baina ya pande mbili.

Kampuni ya GSM ndiyo 'inayoibeba' Yanga iliyokuwa imedhoofika (kitendo cha jambo au hali ya kupungua nguvu ama uwezo). Imefaulu kukubaliana na Bodi ya Ligi Kuu Hispania (La Liga) ili kuiletea klabu yao maendeleo.

Imefichuka kuwa awamu ya kwanza ya mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji wa klabu ya Yanga yamekamilika na kinachofuata ni utekelezaji.

Mwakilishi wa La Liga, Alvaro Paya amesema awamu ya kwanza itajikita katika mambo mawili yaliyofanyiwa tathmini na kuwekwa kwenye ripoti (maelezo muhimu na maalumu) itakayokabidhiwa kwa viongozi wa Yanga.

Paya amesema ripoti iliyokamilika yenye kurasa 400 itatumwa kwa Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Hersi Said ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Yanga. Huyu ndiye atakayeiwasilisha klabuni.

Imeelezwa kuwa ripoti hiyo imefafanua mambo mengi muhimu ambayo kama yakitekelezwa ipasavyo, Yanga itakuwa na mafanikio makubwa baadaye. Mkataba kati ya Yanga na watu hao wa La Liga ulitiwa saini tangu Mei, mwaka huu na pande zote mbili.

Yapo baadhi ya mambo yanayotakiwa kuwekwa wazi na viongozi wa klabu ya Yanga lakini ukimya ndio unaonifanya niandike makala haya.

Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla alisikika akisema angetuma nakala za mkataba huo kwa matawi yote ya Yanga nchini ili kupata maoni yao lakini mpaka sasa kimya ndicho kinachotawala! Je, hajatuma nakala hizo kama alivyoahidi, au ametuma lakini hajapata majibu ya wanachama? Kama ndivyo, ni kwa nini na kimya hicho kina maana gani?

Baadhi ya mambo yaliyo kwenye mkataba huo ni pamoja na La Liga iliyotiliana saini na Yanga kuleta wataalamu wao Tanzania ili kuisaidia Yanga katika mambo mbalimbali ya maendeleo na kandanda.

Uongozi wa Yanga unaonekana kuwa kimya mno kuhusu maendeleo ya klabu na mpaka sasa hajasema lolote kuhusu ahadi yake ya kupeleka mikoani mkataba huo waliosaini ili kupata maoni ya wanachama. Kadhalika hajaitisha mkutano wa wanachama ili kupata maoni yao! Kuna'ni?

Wengi walitegemea kuona wataalamu hao wa kandanda kutoka Hispania watatua nchini lakini hakuna kinachozungumzwa. Je, mkataba ule umeishia hewani au Yanga imeshindwa kukubaliana na baadhi ya mambo yaliyo kwenye mkataba?

Kama ndivyo, kwa nini Mwenyekiti alitia saini kabla ya kuuchunguza kwa makini?

Mpaka sasa yaelekea GSM ndiyo kila kitu katika Yanga. Kampuni hiyo ndiyo inayotafuta wachezaji, kuwasajili na kuwalipa mishahara na marupurupu timu inaposhinda.

Kwa hali hiyo, ni vema usajili wa wachezaji upendekezwe na kusimamiwa na mwalimu kwani ndiye anayejua umuhimu na ubora wa mchezaji wa nafasi mbalimbali katika timu na si vinginevyo. Wajibu wa mwalimu ni kuelekeza aina ya wachezaji anaowataka katika timu yake baada ya kuona eneo fulani halina mchezaji anayefaa katika eneo husika.

Wakati GSM inapokuwa kwenye hekaheka (pilika pilika za huku na kule ambazo zinamfanya mtu asiwe na utulivu), viongozi wa Yanga wamekuwa kama hawapo au wasiohusika na pilikapilika hizo. Aibu iliyoje!

Je, Yanga itaendelea kutegemea misaada ya wenye hela mpaka lini? Itaondokana lini na watu au kampuni zinazoibeba kwa kila jambo ilhali ina viongozi waliochaguliwa na wanachama ili kuiendesha kwa mafanikio?

Ni ajabu iliyoje kuwa Mwakilishi wa La Liga, Paya amesema muda La Liga iliyofanya kazi na Yanga imejifunza mambo mengi ikiwamo Yanga ilivyo na mtaji mkubwa wa mashabiki katika kila pembe ya nchi unaoweza kuwa chachu ya maendeleo ya klabu hiyo.

Maeneo yaliyoainishwa na kuwekwa kwenye orodha ya kuyafanyia kazi kwenye mkataba wa Yanga na La Liga yanahusu nyanja za ufundi, masoko na uongozi. Nani atabisha kuwa Yanga inakalia maendeleo yake bila kujitambua mpaka inazinduliwa na wageni kutoka Ulaya?

"Ukicha kutajwa hutotenda jambo." Maana yake ukiogopa kusemwa na watu ufanyapo jambo hulifanyi asilani. Methali hii hutumiwa kumhimiza mtu anayedhamiria kufanya jambo kisha akawa anaogopa watakavyosema watu wengine. Shime (ari ya kufanya jambo) viongozi.

**marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096**

## HABARI KITAIFA

# TRA yatangaza kuanza stempu za kielektroniki

**Na Frank Maxmillian,** TUDARCo

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imetangaza kuwa kuanzia mwanzoni mwa mwezi ujao, matumizi ya mfumo wa stempu za kodi za kieletroniki (ETS) kwa bidhaa na kazi za filamu na muziki yataanza.

Mbali na filamu na muziki, bidhaa zingine zitakazoguswa na mfumo huo wa kisasa ni pamoja na juisi za matunda, mboga na maji ya kunywa yaliyofungashwa kwenye chupa.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na mamlaka hiyo na kuchapishwa kwenye magazeti mbalimbali, likiwamo Nipashe jana, bidhaa zote zilizoko sokoni na kwenye maghala ya watengenezaji au waingizaji ambazo hazijabandikwa stempu za kodi ya kieletroniki, zinaruhusiwa kuendelea kuuzwa kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

"Hatua hii inafuatia kukamilika na kuanza kwa matumizi ya mfumo huu kwa awamu ya kwanza na ya pili kwa bidhaa za sigara, mvinyo, pombe kali, bia na aina zote za vileo hapo Januari 15, 2019 na kwa bidhaa za vinywaji laini Agosti Mosi, 2019," TRA ilifafanua katika tangazo lake hilo.

Mamlaka hiyo ilibainisha kuwa hadi kufikia Januari 31 mwakani, baada ya tarehe hiyo, bidhaa hizo zote hazitaruhusiwa kuwapo sokoni bila kubandikwa stempu za kodi za kielektroniki.

Ilibainishwa katika tangazo hilo kuwa kila mzalishaji au mwingizaji wa bidhaa tajwa anapaswa kutoa taarifa TRA juu ya idadi ya bidhaa alizonazo ambazo hazijabandikwa stempu za kielektroniki kabla ya tarehe rasmi ya kuanza matumizi ya mfumo huo kwa kujaza fomu maalumu inayopatikana kwenye ofisi za TRA za kila mkoa na katika tovuti ya mamlaka.

"Wadau wote pamoja na umma kwa ujumla wanataarifiwa kwamba bidhaa zote zilizofunagamanishwa kwenye chupa na kazi za filamu na muziki zitakazozalishwa ama ndani ya nchi au kuingiza kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano kwamba kuanzia Novemba Mosi lazima bidhaa tajwa ziwe zimebandikwa stempu.

"TRA inawakumbusha wafanyakazi na wadau wote kuwasilisha taarifa kamili ya chapa zao (brands) na idadi ya stempu za ETS wanazokusudia kutumia kwa mwaka ujao ili kusajiliwa katika mfumo wa usimamizi wa Stempu za Kodi za kielektroniki (ETSMS) na kuagiza stempu kupitia tovuti salama iliyofungamanishwa ndani ya tovuti ya mamlaka," TRA imebainisha kupitia tangazo hilo.

Serikali imelazimika kutumia mfumo huu baada ya kuwapo kwa malalamiko ya muda mrefu kuhusu wizi wa kazi za wasanii huku watumiaji na wazalishaji wa bidhaa kama vile pombe kali na juisi wakilalama kuingizwa na kuzalishwa kwa bidhaa feki katika soko.

# Bil. 3/- zajenga vituo vya afya Kilwa

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitano vya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza kwa nyakati tofauti na wakazi wa Ilulu Njianne katika kata za Tingi na Kivinje kwenye mikutano iliyofanyika wilayani hapa.

"Serikali imetoa Sh. bilioni 3.02 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Masoko ambacho kimekamilika na kinatoa huduma, kituo cha afya cha Pande kinatoa huduma, kituo cha afya cha Tingi kinatoa huduma, kituo cha afya cha Somanga kinatoa huduma na kituo cha afya cha Nanjilinji ambacho ujenzi wake uko kwenye hatua ya ukamilishaji," alisema.

Kuhusu uboreshaji wa afya, Majaliwa alisema Sh. milioni 403 zimetolewa na serikali kuboresha hospitali ya wilaya hiyo iliyoko Kinyonga ikiwamo ujenzi wa duka la dawa na jengo la kuhifadhia maiti. Alisema ujenzi wake upo katika hatua za ukamilishaji.

Pia alisema Sh. milioni 164.7 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa zahanati za Rushungi na Songomnara.

Kwenye ununuzi wa dawa, alisema: "Sh. bilioni 1.43 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo wastani wa fedha za ununuzi wa dawa kwa mwezi ni Sh. milioni 23.9."

Majaliwa ambaye yuko mkoani Lindi kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, alitumia fursa hiyo kuwanadi wagombea ubunge wa majimbo ya Kilwa Kaskazini, Francis Ndulane na Ally Kasinge (Kilwa Kusini), pamoja na wagombea udiwani wa kata za majimbo hayo kwa tiketi ya CCM.

Kwa upande wa maji, alisema Sh. bilioni 7.5 zimetolewa kwa miradi mikubwa ya maji ikwemo mradi wa utafiti wa maji na uchimbaji visima katika vijiji 19; Mradi wa kuboresha huduma ya Maji Kilwa Masoko, ujenzi wa mabomba Somanga na Pande na ujenzi wa mabomba Njia Nne.

"Fedha hizo zimetumika kufanya ukarabati wa mradi wa maji Kipatimu, Ukarabati wa mradi wa maji Mandawa, mradi wa maji ya bomba na uvunaji wa maji ya mvua Mingumbi-Miteja, ukarabati wa mradi wa maji Kijiji cha Kipindimbi, ukarabati wa pampu za mkono 25 katika vijiji 12 vya Kilwa pamoja na Mradi wa Maji ya Bomba Shule ya Sekondari Kinjumbi," alisema.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe | Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store | Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz

# Shule yalia na uhaba walimu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHULE ya msingi Ibinzamata iliyoko Manispaa ya Shinyanga, ambayo inafundisha wanafunzi mchanganyiko wakiwamo wenye ulemavu wa kusikia na kuona, inakabiliwa na upungufu wa walimu maalum.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Seleman Kipanya, alibainisha hayo juzi kwenye mahafali ya Darasa la Saba, huku akibainisha kuwa ina vifaa vyote vya kufundishia zikiwamo mashine za kuchapisha nukta nundu.

Alisema uhitaji wa walimu maalum ni 10 kwa upande wa kufundisha wanafunzi wasioona, huku wanafunzi wasiosikia hakuna upungufu, hivyo kuiomba serikali kutatua tatizo hilo ili wanafunzi wafundishike vizuri na kufaulu masomo yao.

"Wanafunzi hawa wenye uhitaji maalum licha ya kukabiliwa na upungufu wa walimu, wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mitahini yao. Mfano matokea ya darasa la saba mwaka jana, viziwi walifanya mtihani wanane, lakini walifaulu watano, wasioona walifanya nane na walifaulu wote," alisema Kipanya.

Naye mhitimu Naziri Vicent, akisoma risala kwa niaba ya wenzake, alisema walianza masomo wakiwa wanafunzi 117, wavulana 57 na wasichana 60, lakini wamehitimu 110 wakiwamo wavulana 54, na wasichana 56. Alisema walipungua kwa sababu wengine walihamia shule zingine.

Mgeni Rasmi kwenye mahafali hayo, Ofisa Elimu Taaluma Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Wingwila Kitila, akimwakilisha Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Geoffrey Mwangulumbi, alisema tayari wameshaomba walimu hao maalum ili kuondoa upungufu uliopo.

Pia alitoa wito kwa wanafunzi hao wajichunge wakiwa nyumbani mwao na kuacha kuzurura ovyo mitaani wakati wakisubiri matokeo ili wakutwe wakiwa salama hasa kwa wanafunzi wa kike.

# Kampuni madini kumwaga ajira 1,200

**Na William Budoya,** MPANDA

KAMPUNI ya Mgodi wa Katavi inatarajia kuajiri watu 1,200 wakati wa kuanza shughuli zake za uchimbaji na uchenjuaji wa madini Desemba, mwaka huu, baada ya kusimama uendeshaji kwa miaka mitatu.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Mahmood Abdul Razaq Yass, alisema hayo kwa njia ya mkutano wa video kutoka Muscat, Oman kwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera alipotembelea mgodi huo mapema wiki hii. Yass alisema shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini zitatanguliwa na mafunzo ya wafanyakazi ambayo yatawajengea uwezo wa kufanya kazi katika mitambo ya uzalishaji.

Pia alionyesha mpango wake wa ajira kuwa kwa hatua za awali ataajiri wafanyakazi 500 lakini kadri mgodi utakavyozalisha vizuri kwa faida, kampuni itaendelea kuajiri wafanyakazi hadi 1,200 ambao watajumuisha wenyeji na wageni

Kwa kuzingatia umuhimu wa mgodi huo, Homera aliuhakikishia uongozi wa kampuni hiyo kuwa upatikanaji wa visa na vibali vya kufanya kazi nchini kwa wageni, zitashughulikiwa na kutolewa haraka ili kuwawezesha wageni kufanya kazi.

Homera pia alisema changamoto zote zinazoikabili kampuni hasa umeme na barabara zitashughulikiwa na serikali kwa haraka ili kuijengea kampuni mazingira rafiki ya uwekezaji.

Mkuu wa mkoa alionyesha hatua ambazo tayari amechukua kuhusu umeme kwa kumwandikia Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kupanga kuupatia mkoa umeme wa kutosha kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Hata hivyo tayari serikali inaendelea na mradi wa gridi ya taifa ambapo mradi utakapokamilika utapunguza matatizo ya umeme na kukidhi mahitaji mbalimbali ya mkoa wa Katavi.

Kampuni ya Mgodi wa Katavi ambayo inamilikiwa na Alhoogani International Group, ilianzishwa 2012 na kusajiriwa na Wakala wa Leseni na Majina ya Biashara (BRELA) kufanya shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini Tanzania katika mkoa wa Katavi. Kampuni hiyo ilisitisha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini mwaka 2017 kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 ambayo haikuruhusu kusafirisha malighafi na makinikia.

Lakini kutokana na sheria mpya ya madini ya 2020 kifungu cha 129 ya Agosti 28, 2020 imeruhusu kusafirisha Makinikia nje ya nchi yenye kiwango kisichopungua asilimia 20



Mgombea ubunge wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), akiteta jambo na mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Simbo, wilayani Igunga, mkoani Tabora, wakati wa kampeni zake za uchaguzi mkuu juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi watamba udahili shule maarufu

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Hazina wametia fora kwa kuongoza kwenye usaili wa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule maarufu nchini.

Mkuu wa Shule hiyo, Omari Juma, alisema jana kuwa wanafunzi wengi wa shule hiyo waliokwenda kufanya usaili kwenye shule zenye majina makubwa, wameongoza na kupata nafasi za kujiunga kidato cha kwanza.

Alitoa mfano kuwa mwanafunzi aliyeongoza kwenye usaili kwenye shule maarufu ya Feza Boys, Alice Edward, ametoka Hazina na kwamba wanafunzi wa shule hiyo wamekuwa wakiongoza kila mwaka kwenye usaili.

Alisema kwenye usaili wa mwaka huu wanafunzi sita wa Hazina wamefanikiwa kufanya vizuri zaidi kwenye usaili na kujiunga na shule za Marian zilizoko Bagamoyo mkoani Pwani.

Juma alisema wanafunzi sita wa Hazina wamefanikiwa kufanya vizuri zaidi na kujiunga na shule za Feza wakati wanafunzi wengine tisa wamefanya vizuri na kujiunga na shule ya wavulana ya Shamsiye.

"Mwaka 2019 tulipeleka wanafunzi wengi sana kwenye shule hizo na waliongoza na wazazi wengi wanapenda sana watoto wakimaliza shule ya msingi wakasome shule nzuri ndiyo sababu wanapenda kuwaleta hapa Hazina," alisema

Mzazi ambaye mtoto wake ameongoza kwenye usaili shule ya Feza alielezea kufurahishwa kwake na matokeo hayo na kufanikiwa kupata udahili kwa kuwa wanafunzi walikuwa wengi kupita kawaida.

"Wanafunzi wanaofanya udahili wanafikia 6,000 nafasi zilizopo ni 100 hivyo kupata nafasi pale ni ushahidi kwamba hapa Hazina wanafunzi wanaandaliwa vizuri sana," alisema

Alisema amefurahi kuona mtoto wake amepata shule ambayo ilikuwa ndoto yake na amewashukuru walimu na wafanyakazi wa shule ya Hazina kwa namna walivyomuandaa mwanafunzi huyo.

"Kwa kweli shule ya Hazina imekuwa ikifanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa na kwa kweli wamewaandaa vyema wanafunzi na kushinda kwenye usaili kwenye shule hizi zenye majina makubwa ni ushahidi wa namna Hazina ilivyo shule bora nawashukuru na kuwapongeza sana," alisema





# Polisi waonya waandishi mavazi vyama vya siasa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limewaonya waandishi wa habari kuacha kuvaa mavazi yenye rangi za vyama ili kuepuka kuleta vurugu wakati wa uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Jumatano ijayo.

Msemaji wa jeshi hilo, David Misime, alitoa onyo hilo jana jijini Dodoma wakati wa mkutano wa Chama cha Waandishi wa Habari wa Nchi za Kusini mwa Afrika (MISA).

Misime alisema waandishi wakivaa nguo zenye rangi inayofanana na chama fulani, inaweza kuwaletea matatizo wakati wa kuripoti uchaguzi huo.

Alisema waandishi wanapaswa kuwa makini katika suala hilo ili kujiweka sawa katika siku ya kupiga kura.

Misime aliitaka Kamati ya Maridhiano baina ya wanahabari na vyombo vya ulinzi na usalama iwe na mawazo chanya huku akisisitiza kila mmoja kutimiza majukumu yake.

Alisema yale watakayojadili katika kikao hicho, yanatakiwa yawe na mlengo mmoja kwa kuwa wao hawana upande wowote.

"Sisi Jeshi la Polisi tunasema wanaotaka haki lazima pia wajue na wajibu wao, maana tunasikia watu wanahubiri haki lakini wajibu hawasemi," alisema.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Prosper Kwigize, alisema miaka ya karibuni, uhusiano kati ya vyombo vya ulinzi na usalama na waandishi wa habari umeimarika.

"Waandishi wa habari ni daraja, wanatoa taarifa katika taasisi mbalimbali na kuzipeleka katika umma, hivyo wanatakiwa kufanya kazi katika mazingira mazuri na ya usalama," alisema Kwigize.

Mwakilishi wa MISA, James Marenga, alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kukaa kikao cha pamoja na Jeshi la Polisi Agosti mwaka huu.

Alisema baada ya kujadili mustakabali wa waandishi wa habari katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, walikubaliana mapendekezo manane, mojawapo ni waandishi kulindwa na polisi.

Marenga alisema walichukua hatua ya kujadiliana na jeshi hilo baada ya kuona madhara ambayo yamewahi kutokea katika uchaguzi uliopita ambapo baadhi ya waandishi wamekuwa wakipigwa na wengine kuuawa na polisi.

Alisema mengine ni waandishi kuvaa sare pamoja na vitambulisho ambavyo vitawatambulisha katika uchaguzi huo.

Alisema waandishi watatakiwa kupeleka picha pamoja na majina yao katika Jeshi la Polisi ili askari wa jeshi hilo watakapokuwa wakipambana na wahalifu katika uchaguzi, wawatambue kwa urahisi.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, akizungumza na wazazi na walezi kwenye mahafali ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Makole, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# CUF yaahidi neema Kondoa

**Na Peter Mkwavila,** KONDOA

CHAMA cha Wananchi (CUF) Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma, kimeahidi kuwaondolea wananchi adha ya kutembea umbali wa kilomita 11 kufuata huduma za matibabu.

Katibu wa chama hicho Wilaya ya Kondoa Mjini, Juma Athumani, alitoa ahadi hiyo jana alipomnadi mgombea udiwani Hamidu Mkopi wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika viwanja vya Chang'ombe.

Athumani alisema wananchi wa Kata hiyo wakimchagua mgombea wao huyo, watahakikisha wanawaondolea kinamama adha ya kutembea umbali wa kilomita 11 kufuata huduma ya mama na mtoto ambayo inapatikana katika Kijiji cha Chololo Wilaya ya Kondoa Vijijini.

Katibu huyo pia aliwataka wananchi wa kata hiyo kutofanya makosa kwa kuchagua viongozi ambao hawana sera za kuwaletea maendeleo, ambayo yanahitajika kwa Watanzania wote bila kujali itikadi zao.

"Kichagueni chama cha CUF ili kikawaondolee kero ambazo zimekuwa sugu kwenye maeneo mnayoishi ikiwamo maji, umeme, zahanati, elimu, ufugaji na upande wa kilimo pia," alisema.

Mgombea udiwani, Hamidu Mkopi, aliwaomba wakazi wa Kata ya Chang'ombe kumchagua ili afanikishe kutatua kero walizokuwanazo ikiwamo ya maji.

Alisema kwenye kata hiyo, kero kubwa iliyopo ni upatikanaji wa maji salama ya uhakika ambayo hivi sasa yanapatikana kwenye visima vya kienyeji ambavyo hata wanyama wanayatumia.

"Ninaomba msifanye makosa kwa kuchagua uzuri wa jina la chama, bali chagueni mtu ambaye atawatatulia kero kama hii ya upatikanaji wa maji salama pamoja na suala la kutembea umbali mrefu zaidi ya kilometa 11 kufuata huduma za afya," alisema.

Alisema akipewa ridhaa hiyo kuwa diwani, atahakikisha fursa za mikopo inayotolewa na halmashauri inapatikana kwa vijana, watu wenye ulemavu na kina mama.

# 'Serikali itaendelea kuzikarabati shule'

**Na Peter Mkwavila** DODOMA.

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amesema serikali inaendelea kukarabati majengo yake ya shule ili kuondoa vikwazo katika miundombinu hiyo.

Mavunde aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya darasa la saba katika Shule ya Msingi Makole jijini Dodoma.

Wanafunzi wa shule hiyo kupitia risala yao, walisema kero iliyopo shuleni huko ni kuwapo kwa mwingiliano wa watu ambao mara nyingi wamekuwa wakipita karibu na madirisha ya madarasa na kusababisha kukosa usikivu wakati wanapokuwa darasani kwa kuwa shule hiyo haina uzio.

Leah Herman, akisoma risala hiyo kwa niaba ya wanafunzi hao, alisema wakati mwingine wanafunzi humwagiwa mchanga madirishani na kupigiwa kelele na vijana wanaopita karibu na madirisha na kusababisha hofu ya usalama wao.

Alisema Shule ya Msingi Makole itaondokana na kero hiyo ikiwa serikali kwa kushirikiana na jamii wakikarabati na kujenga miundombinu hiyo.


Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Veronica Mrope, alisema kero hiyo mwingiliano wa watu ambao mara kwa mara wamekuwa wakipita, inaondoa utulivu wa wanafunzi darasani.

"Tatizo shule yetu ipo barabarani, na wengi wanaopita hapa ikiwamo magari, waendesha bodaboda na wapita kwa miguu, lakini kibaya zaidi kuna baadhi ya vijana wamefikia hatua hata ya kuwamwagia mchanga wanafunzi wanapokuwa madarasani, hii yote ni kwa sababu hatuna uzio ambao wa kuzuia," alisema.

Alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,100, akiwaomba wazazi na serikali kujitoa kwa hali na mali ili kufanikisha ujenzi wa uzio ambao utasaidia kuondokana na kero hiyo.

Akijibu maombi hayo, Mavunde alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu, itahakikisha inawaondolea kero hiyo ambayo imekuwa ikisababisha wanafunzi kukosa haki zao za kimsingi za usikivu na amani wanapokuwa darasani.

Aliwataka wahitimu kujiepusha na anasa ambazo zitawaletea madhara na kujikuta wakishindwa kuendelea na masomo.



# Mwinyi aahidi mishahara minono

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema akipata ridhaa ya kuongoza Zanzibar, serikali ya awamu ya nane itawaangalia kwa karibu watumishi wa umma katika kuboresha mishahara na posho zao.

Alitoa ahadi hiyo katika mkutano wa kampeni Mkoa wa Magharibi zilizofanyika Dole Wilaya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema ili kufanikisha dhamira hiyo, serikali inakusudia kujiimarisha kiuchumi na kuwataka wafanyakazi kila mmoja mahali alipo kuwajibika ipasavyo katika kazi.

Dk. Hussein alisema katika dhamira hiyo ya kukuza uchumi, serikali atakayoiongoza pia itapitia pensheni za wastaafu kwa lengo la kuziboresha. Aliipongeza serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kufanya kazi kubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015-2020.

Alisema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji huo katika wilaya zote za mkoa huo ni uimarishaji wa sekta za elimu, afya, miundombinu ya barabara na uapatikanaji wa huduma za maji safi na salama.

Alisema sekta ya afya imefanyiwa kazi kubwa ambapo vituo mbalimbali vya mama na mtoto pamoja na vya kujifungulia vimejengwa na kuimarishwa.

Dk. Mwinyi alisema serikali ijayo inalenga kukamilisha kazi iliyobaki ya kuondoa miundombinu ya maji iliyochakaa na kuweka miundombinu mipya na kusambaza katika maeneo ambayo hivi sasa haipo.

Akizungumzia tatizo la ajira, mgombea huyo alisema kila mwananchi anayehitaji kufanyakazi, atapata fursa ya kufanya hivyo, akibainisha mpango wa serikali wa ajira 300,000, zikiwamo zilizo rasmi, zisizo rasmi pamoja na vijana wengine kuwezeshwa kimafunzo ili kujiajiri. Dk. Hussein alisema serikali ijayo itasimamia utaifa na kuondokana na ubaguzi wa matabaka katika aina zote, iwe kidini au majimbo.

Vilevile, alisisitiza umuhimu wa wananchi na wanachama wa CCM kuendelea kuilinda amani iliyopo na kuwataka kuwa watulivu na kuviachia vyombo vya dola kufanya shughuli zake.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, aliwakumbusha wananchi wa Zanzibar umuhimu wa kulinda na kuyaendeleza Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, kwa kuwa yalilenga kuwakomboa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba ili wawe huru.

Dk. Shein ambaye pia ni Rais wa Zanzibar, alisema kabla ya Mapinduzi ya 1964, wananchi wanyonge wa Zanzibar walidharauliwa, kupuuzwa na kubezwa katika nyanja zote na kubainisha kuwa kufanyika kwa mapinduzi hayo kuliazimia kuwaweka pamoja na kushikamana.

Alisema hakuna mbadala wa mapinduzi hayo na hivyo akawataka wananchi wayatunze na kuyadumisha, akibainisha watu wote kuwa ni sawa. Alisema amani, umoja na mshikamano uliopo nchini umeletwa na mapinduzi na hivyo kutoa fursa za upatikanaji wa haki zikiwamo za matibabu bora na kumiliki ardhi.

## Mgombea: Wananchi hawatakula dagaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar, Said Sudi (AAFP), amesema akipata ridhaa kuwa Rais, atahakikisha wananchi wa Zanzibar hawali 'dagaa tonge'.

Katika mkutano wake wa kampeni visiwani hapa jana katika viwanja vya Magirisi, mgombea huyo alisema Zanzibar imezungukwa na bahari, hivyo atahakikisha samaki wanapatikana kwa wingi na watakuwa na bei nafuu ili kila mwananchi ale samaki.

Alisema wananchi wanakula dagaa tonge kwa sababu hawana uwezo wa kununua samaki kwa ajili ya mahitaji ya chakula.

Sudi alisema akiwa Rais wa Zanzibar, atahakikisha dagaa wanalovuliwa wanaanikwa na kuuzwa nje ya nchi kama vile Congo na maeneo mengine.

"Nikiwa Rais, hamtakula dagaa tonge na badala yake mtakula samaki wenye minofu," aliahidi mgombea huyo.

Pia, alisema atahakikisha anaimarisha uchumi wa nchi ili wananchi wa Zanzibar kuwa na maisha mazuri.

Mgombea huyo aliwataka wananchi kudumisha amani ya nchi na kuwasisitiza kwenda kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu.

Alikumbusha kuwa wananchi hawapaswi kwenda kupiga kura Oktoba 27 kwa sababu kura hiyo ni kwa watu maalum kama ilivyoelezwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).



Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Zanzibar Dk. Ghirmay Andemichael (kushoto), akikabidhi mashine ya kupumilia kwa Mkurugenzi Mkuu Wizara Afya Zanzibar, Dk. Jamala Adam Taib, ikiwa ni sehemu ya vifaa vilivyotolewa msaada na shirika hilo kwa Wizara hiyo, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Balozi Iddi atoa angalizo kesi za dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Iddi, amewataka watendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar kuelewa kwamba wana jukumu la kuhakikisha kesi zinazohusiana na dawa za kulevya zinapatiwa ufumbuzi unaostahiki.

Alisema hatua hiyo mbali ya kuirejeshea imani ya jamii juu ya hatua za mapambano dhidi ya janga hilo, pia itadhibiti mmong'onyoko wa maadili kwa kundi kubwa la vijana linaloonekana kuangamia kwenye matumizi ya dawa hizo hatari kwa afya na mazingira.

Balozi Iddi aliyasema hayo katika kikao cha mwisho cha wajumbe wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar akiwa Mwenyekiti wake kilichofanyika Forodhani kikiambatana na hafla ya kuagana.

Alisema wapo baadhi ya watu wanaokamatwa wakituhumiwa kuhusika na uingizaji, usambazaji pamoja na uuzaji wa dawa za kulevya lakini kesi zao zimekuwa zikisuasua kwa kuchukua muda mrefu na matokeo yake zinashindwa kupatiwa uamuzi huku ongezeko la janga hilo likiathiri jamii.

Alisema ili janga hilo liondoke au kupungua, ni lazima watendaji wanaohusika na kusimamia mapambano hayo wajitolee kuona kadhia hiyo inasahaulika huku wakimtanguliza Mungu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud Mohamed, kwa niaba ya wajumbe wenzake, alimpongeza mwenyekiti huyo wa tume hiyo kwa umahiri wake kuiongoza kwa mafanikio makubwa.

Waziri Aboud alisema umahiri huo kwa kiasi kikubwa umepelekea taasisi hiyo inayosimamia udhibiti wa dawa za kulevya kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



CARD B UMELIVURUGA MWENYEWE
Ukurasa.14

JUMAMOSI OKTOBA 24, 2020



# "USITUUMIZIEE"

# Mashabiki Yanga wamlilia Wema

STAA wa filamu nchini, Wema Sepetu, amezidisha joto katika mitandao ya kijamii, baada ya mashabiki wa Yanga kumtahadharisha kuwa mbali na mchezaji wa timu yao, Carlos Carlinhos.

Hivi karibuni zilisambaa picha zikimuonyesha mrembo huyo akiwa na Carlinhos, katika duka moja la mavazi na mapambo ya nyumbani.

Licha ya mke wa Carlinhos, anayeitwa Vanessa ambaye amezaa naye mtoto mmoja kuweka ujumbe mzito mtandaoni, akitaka kuambiwa ukweli, mashabiki wa Yanga nao wameonya ukaribu wao huo ambao unawapa hofu unaweza kuharibu umakini wa mchezaji wao.

Hata hivyo, Wema katika posti zake katika ukurasa wake wa Istagram, hakusema mengi badala yake aliandika "Daima mbele, nyuma mwiko"

Baadhi ya mashabiki hao walisema wanachojua kwa Wema huwa hakai mbali kwa wanaume 'Handsome' na kuibuliwa kwa picha hizo zinaweza kuwagharimu kutokana na mchezaji wao kushuka viwango.

"Sisi hatuna ukweli kama wana uhusiano au la, lakini wasiwasi wangu kama Wema Sepetu, akijiweka karibu kwa Carlinhos, tunaweza kuona mabadiliko na kugharimu timu," alisema Juma Akida.

Mchangiaji mwingine aliandika "Usituumiziee, Wema unanifanya nikumbuke maneno ya shuleni Usituumizieee tunamtegemea,"

Wema anasifika kwa kujihusiha kimapenzi na mastaa tofauti wa kiume, akiwamo mwanamuziki Diamond Platnumz, Idris Sultan, Calisah, Mr Blue  na marehemu Steven Kanumba.

BASI SAWA

## Duh! Kamganda Harmonize

HILI ni shavu la nguvu! Kijana anayejiita Followzee, kutoka Mbagala Jijini Dar Es Salaam, anapata umaarufu baada ya kufananishwa na msanii mkubwa nchini, Harmonize.

Followzee, amesema yeye anajiona kama mwanafamilia wa lebo ya Konde Gang, kwani yeye pia anatoka ,Mkoa wa Mtwara kama alivyo Harmonize na Ibraah Tz.

"Mimi sio chawa wala mdananda wa Harmonize, huu ndiyo mtindo wangu wa nywele sio kama namuiga kuna muda huwa nasuka pia nazipaka rangi, hata jila la pacha sijiiti bali wananiita watu kwa kufananishwa naye, wengi wananiita Konde Boy Jeshi au Tembo na ndiyo majina ambayo anayotumia Harmonize mwenyewe" amesema.




## Huyu Meja Kunta mpya

MWANAMUZIKI wa Singeli, Meja Kunta, sasa amepata muonekano mpya baada ya kufanyiwa upasuaji na kuwekwa jino bandia.

Meja Kunta, ambaye alikuwa na pengo la juu upande wa kushoto, amepata umaarufu kutokana na kupiga aina tofauti ya muziki huo tofauti na wengine.

Hata hivyo, msanii mwenzake Marioo, alimpiga kijembe akimwambia amepata pesa kidogo tu, tayari amekwenda kubadilisha jino.





## Ole wenu 'One Time' kuisikiliza

SIKU chache baada ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kuufungia wimbo wa 'One Time' wa mwanamuziki, Lady Jaydee, uongozi wa msanii huyo umesema bado hajaona kosa hadi kuchukuliwa kwa hatua hiyo.

Akizungumzia taarifa hiyo kupitia EATV, Meneja wa msanii huyo Mx Carter, amesema wao kama wamiliki wa wimbo huo hajaona kosa, kwani vitu vinavyolalamikiwa ni jambo la kawaida katika jamiii.

"Tuliitwa kwa sababu kuna vitu wao kama BASATA waliona havijakaa sawa, tukaitikia wito kwa Lady Jaydee kwenda ili kuzungumza nao, na leo tukapokea barua rasmi ya kuamua kuufungia na hautoruhusiwa kupigwa kwenye vituo vya Radio TV na kwenye mitandao kama wa YouTube" ameeleza MX Carte.

Ameongeza "Kuna mstari ambao nisingependa kuutaja ila wanasema unahamasisha vitu ambavyo sio maadili ya Kitanzania, ila kwa sisi tulivyoona haukuwa unahamasisha kwa sababu ni vitu ambavyo vipo na vitu vya kawaida" ameongeza MX Carte.



## Duma kawa kidume mahaba

UKISIKIA mtu anadeka, ndivyo anavyofanya mchumba wa mwigizaji wa Bongo Muvi, Duma, kwani hivi karibuni ametamba kwamba mapenzi anayopewa yamemchanganya akili.

Kisha mrembo huyo anayeitwa Mishi Dorah, raia wa Kenya, amesema licha ya wabongo kuchamba katika mitandao ya kijamii, hawezi kuchoshwa na badala yake atazidisha mahaba.

"Duma ni 'mtanashati na ndiyo mwanamume wa ndoto zangu, nilitamani kuwa naye na mtu mzuri sana kwangu, tayari nimeshafika kwao ila nimegundua kuna mawifi wengi na wanachamba sana ila nimefurahi" amesema Mishi Dorah.



## Moto nje ya Yamoto Band

**Na Adam Fungamwango**

UNAIKUMBUKA Yamoto Band? ile bendi ya Viserengeti Boys vilivyotamba miaka ile na kutoa ngoma kali zilizotishia wasanii wengi waliokuwa mastaa kipindi hicho.

Ni bendi iliyokuwa chini ya Mkubwa Fella, ambayo ilikusanya vijana wadogo wenye vipaji vya hali ya juu ambao walitoa ngoma kali ambazo hadi leo zikipigwa bado zinaendelea kuwasisimua mashabiki kwenye hafla mbalimbali.

Walikuwa ni vijana wanne ambao wakiungana na Mkubwa Fella walikuwa wanaunda kitu kinachoitwa 'Mkubwa na Wanawe'. Sidhani kama kuna shabiki wowote wa muziki anaweza kusahau ngoma zilizovuma kama 'Cheza kwa Madoido', 'Nitakupwelepweta', 'Niseme', 'Nisambazie raha' na nyingine nyingi.

Ni bendi iliyoanzishwa katikati ya miaka ya 2000 na kujizoelea mashabiki wengi.

Ni bendi ilivuma sana, lakini ikavunjika kirahisi sana. Hakuna aliyetegemea na hakuna sababu yoyote ile yenye mashiko inayoeleza kuvunjika kwa bendi hiyo.

Tayari wasanii hao walishakuwa maarufu, hivyo kila mmoja akaondoka. Na kama ilivyotegemewa na wengi ni kuwa kila mmoja angekwenda kuonyesha kipaji chake huko anakokwenda.

Na kweli wengi wao wamekuwa wakitoa ngoma kali nje ya bendi ya Yamoto.

**ASLAY ISIHAKA**

Kwa sasa anaitwa Aslay Ishaka, lakini hapo zamani alikuwa akiitwa Dogo Aslay kutokana na kuwa na umri mdogo wakati anaanza mambo ya muziki.

Alikuwa ndiyo mwimbaji kiongozi wa Yamoto Band, na alikuwa kioo au staa wa bendi.

Ilitegemewa kuwa akitoka ataendelea kutamba. Na kweli alipotoka alitoa ngoma nyingi sana.

Lakini ngoma za hivi karibuni ambazo zinamfanya kuendelea kutamba ni 'Nichombeze', 'Nainjoi', 'Mchepuko', 'Mateka' na nyingine nyingi ambazo zimemfanya kuendelea kutesa japo yupo nje ya Yamoto Band.

**MAROMBOSO**

Ni mmoja wa wasanii waliokuwa na mvuto kwenye bendi ya Yamoto. Yeye alipoondoka alisuasua kidogo, lakini baada ya kusimama sawa ikawa balaa.

Kwa sasa anatamba na ngoma kama 'Haijakaa Sawa', 'Tamba', 'Sina Nyota', na zinginezo. Hizi ni za karibuni tu. Naye ni mmoja wa wasanii ambao wanaiwakilisha Yamoto Band nje ya bendi hiyo.

**ENOCK BELLA**

Hakuna aliyetegemea kama akitoka Yamoto Band atatamba. Ilionekana kama vile anatembelea nyota za wenzake. Wapi bwana. Baada ya kila mmoja kula kona kivyake, na yeye pia hajapoa.

Wiki moja tu iliyopita ametambulisha ngoma yake mpya aliyoiita 'Chukua'.

Mbali na pini hilo, tayari alishakonga nyoyo za mashabiki wengi wa muziki alipotoa pini zingine kama 'Peke Yangu', 'Sauda', 'Hana Huruna', 'Ngoja Kidogo' na nyinginezo.

**BEKA FLAVOUR**

Huyu ni mmoja wa wasanii wenye sauti tamu aliyekuwepo kwenye Yamoto Band.

Nadhani kipaji hiki kisingejulikana sana kama bendi hii isingesambaratika.

Amejipambanua kuwa msanii mwenye uwezo wa hali ya juu na kujizoelea mashabiki wengi.

Ngoma zake kali ni 'Sikinai', 'Unanimaliza', 'Tuwe Sare', 'Sarafina', 'Kibenteni' na nyinginezo.

## Damu Yangu; Ndivyo sivyo, sivyo ndivyo

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ina mambo mengi ya ajabu ambayo wakati mwingine ukisimulia unaweza kushangaa kuwa imetokeaje. Lakini katika hii dunia kila kitu kinawezekana hata kile ambacho unaona kwa hali ya kawaida haiwezekani. Hii yote ni mipango ya Mwenyezi Mungu.

Ukitaka uamini hivyo fuatilia filamu ya 'Damu Yangu'. Ni filamu inayotukumbusha kuwa Mungu akipanga lake, binadamu hawezi kupangua.

Imechezwa na wasanii Majuto Kipulilo, Julius Mwiga, Mwajuna Omari, Rajab Wajala, Blandina Maganga, Johari Kassim na wengineo.

Inaanza kuonyesha kijijini ambapo mama mmoja akiagana na binti yake ambaye anakwenda mjini kutafuta vibarua baada ya kuchoshwa na maisha ya shamba.

Hata hivyo, mama huyo anayeitwa Anita anamwambia binti yake Scolla kuwa ametoka kwenye ukoo wenye uwezo mkubwa, ila mpaka sasa hajui baba yake alipo.

Binti anakwenda mjini na kwa bahati nzuri anapata kazi za ndani, maarufu kama 'hausigeli'. Alipata kazi kwa Mr. Gobos, mzee tajiri ambaye alikuwa akiishi na binti yake mmoja tu aitwaye Stella.

Stella ni msichana aliyedekezwa na baba yake kiasi cha kufanya chochote alichotaka.

Ujio wa Scolla aliona kama anaweza kumnyang'anya haki yake, kwani baba yake alionekana kumpenda pia binti huyo kama mtoto wake, japo ni hausigeli.

Stella akawa anamnyanyasa Scolla, ingawa mwenyewe alikuwa hajali hilo. Stella akawa anafanya mpango wa kutaka Scolla afukuzwe kazi.


Siku moja Scolla alipata barua mama yake mgonjwa, hivyo alilazimika kuletwa mjini kwa ajili ya matibabu. Bosi Gobos aligharamia. Wakati yupo hospitali mama Scolla amelazwa, bosi alifuatana na binti kwenda kumuona mama yake. Cha ajabu ni kwamba walipoonana wakatambuana.

Gobos alimuuliza kwa nini alikimbia na mtoto wake? Anita mama Scolla anaanza kuhadithia kilichotokea.

Ni kwamba Anita alikuwa hausigeli na Gobos miaka mingi nyuma. Gobos na mkewe walichelewa mno kupata mtoto. Kutokana na hali hiyo, ilibidi wamuombe Anita akipata mtoto wamchukue wamuasili awe wao. Mumewe Anita alikubali na mtoto akapatikana, lakini miaka michache baadaye mzee huyo na mkewe wakapata mtoto wao.

Hiyo ilimfanya mumewe Anita achukie kwani alijua mtoto wake ndiye atakayerithi mali, kwa hiyo akamshauri mkewe wamuue mtoto halisi ya mzee Gobos ili abaki yule wao.

Anita hakukubaliana na hilo, hivyo akatororoka na mtoto wa bosi wake halisi ili asiuawe na kumuacha wa kwake kwani alijua hatouawa na mumewe. Wakati huo wote Gobos na mkewe hawakuwapo. Mume wa Anita aliyekuwa akiishi na mzee huyo hayo baada tukio hilo akatoroka. Mke wa Gobos liporejea na kukuta Anita ametoroka na mtoto wake akaanguka na kufariki.






# Rihanna kumbe nawe unachukia?

MSANII nyota wa muziki wa Marekani, Rihanna, ameungana na mastaa wengine duniani kupinga mauaji ya waandamani nchini Nigeria.

Vijana wa nchi hiyo kwa wiki kadhaa wamejimwaga mitaani kupinga kikosi cha kupambana na ujambazi maarufu kama Sars, wakidai kinaua watu kiholela na kutesa.

"Siwezi kuamini kuona mauaji yakiendelea na kuathiri mataifa katika sayari yetu, lazima tuwalinde watu, tuwe na hofu," amesema Rihanna.



## Jeff Bridges ajitangazia ugonjwa

MWIGIZAJI wa Hollywood, Jeff Bridges, ametangaza kuugua ugonjwa wa lymphoma.

Nyota huyo alitumia ukurasa wake wa Twitter, kutangaza habari hiyo mbaya kwa mashabiki wake.

Msanii huyo alichukua fursa hiyo kuwashukuru wafuasi wake na raia wa Marekani kwa kumpa ushirikiano na kuwaomba kutumia haki yao ya kupiga kura kumpata kiongozi bora wa nchi hiyo.


## Card B umelivuruga mwenyewe

RAPA mwenye mafanikio makubwa Marekani, Cardi B, amefuta ukurasa wake wa Twitter, siku chache baada ya mashabiki wake kumjia juu kuhusu kurudiana na mume wake Offset.

Card B aliweka ujumbe katika ukurasa wa Istagram, akisema aliamua kuchukua hatua hiyo baada ya watu kumwashia moto wakimtuhumu mwanamuziki huyo kuwa kigeugeu.

"Kuna kijana mmoja wa miaka 15, aliniambia ninaishi kama alivyo mama yake, nilipoangalia video yake niliona kama natoka shemu fulani," amesema Card B.





## Burna Boy akasirishwa mauaji

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Burna Boy, amejitokeza na kulaani mauaji ya waandamanaji wanaopinga kikosi cha polisi cha Sars.

Vijana kadhaa walipoteza maisha baada ya kushambuliwa na maofisa wa usalama wakati wakijaribu kuvunja maandamano mjini Abuja.

"Waliondoa kamera za CCTV, walizima taa na wameua watu na kuchukua miili yao. Serikali nzima inapaswa kuachia ngazi , aliandika kupitia ukurasa wake wa twitter.

## Mwimbaji wa Injili avamiwa

MWIMBAJI wa muziki wa Injili kutoka Ghana, Celestine Donkor, amepatwa na mkasa mzito baada ya majambazi kumshambulia na kumjeruhi.

Amesema watu hao waliingia kwa nguvu ndani ya nyumba yao, kisha kuwafungia ndani ya chumba yeye na mume wake kwa masaa kadhaa.

"Walitufungia chumbani mimi na mume wangu,kisha walienda chumba cha watoto, huko mbinti yangu alijaribu kupiga kelele lakini alidhibitiwa," amesema.





Mkurugenzi wa Huduma za Maabara wa TMDA, Dk. Danstan Hipolite, akitoa maelezo kwa Wajumbe wa Bodi ya TMDA waliotembelea maabara ya Kanda ya Ziwa.

# Mkurugenzi TMDA na simulizi maajabu wanavyowavuta wageni kuja kujifunza

## ■Miaka minne mageuzi ya dawa 200%

**Na Mary Geofre**

MNAMO mwaka 2015, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), ambayo zamani ilijulikana TFDA kwa maana ya Mamlaka ya Chakula na Dawa - TFDA, iliandaa mpango maalum katika maeneo ya kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, ili kulinda afya ya jamii.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, anasema waliweka mifumo na taratibu za ndani za utoaji huduma bora, ili wakidhi mahitaji na matarajio ya wateja kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Anataja maeneo 12 wanayofanyia mageuzi makubwa yanayogusa ubora, usalama wa dawa, vifaa na vitendanishi, katika mtazamo wa ongezeko la wafayanyabiashara kuelewa matakwa ya kisheria yanayoshikamana na bidhaa husika.

Fimbo anaeleza kuwa mamlaka hiyo husajili maeneo ya biashara za bidhaa tajwa, lengo ni kutambua maeneo zinakozalishwa, hifadhi, usambazaji na uuzaji.

"Mfumo huu husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa," anasema Fimbo, anayedokeza katika katika miaka minne iliyopita, wamesajili maeneo mapya 32,860 ya biashara za bidhaa zinazodhibitiwa.

Hapo anataja maghala ya bidhaa, maeneo ya usambazaji, maduka ya jumla na rejareja kwa bidhaa hizo, utoaji msaada wa kiufundi kwa viwanda vilivyopo na kuanzisha viwanda vipya 12.

Katika orodha iliyopo anataja viwanda vya dawa za binadamu saba; dawa za mifugo nne; na kimoja mahsusi kwa ajili ya vifaa tiba.

Pia, anadokeza jumla ya maeneo 18,753 yanayojihusisha na biashara ya chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi yalikaguliwa, ambayo yanajumuisha viwanda vya usindikaji, maghala ya kuhifadhia bidhaa, hospitali, vituo vya afya, magari ya kusafirisha bidhaa, maduka ya jumla na rejareja na machinjio mbalimbali.



Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mkurugenzi Fimbo anasema, ni ukaguzi uliolenga kuhakiki ubora wa majengo, mifumo ya utengenezaji na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, hifadhi na uuzaji bidhaa, hivyo ukaimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa.

### UDHIBITI MIPAKANI

Fimbo anasema, katika kuharakisha utoaji mizigo bandarini, mamlaka imeweka wakaguzi wake wanaofanya kazi kila siku, pia ina mfumo wa kieletroniki unaomuwezesha mteja kutuma maombi, malipo popote na kupata kibali ndani ya saa 24.

Anasema, kuna mafanikio makubwa kuwezesha uingizaji bidhaa nchini ndani ya miaka minne, kwa kiwango cha asilimia 203, katika mwaka, kuanzia 2015/16.

Mkurugenzi anasema, katika mpango wa ufuatiliaji ubora wa bidhaa sokoni, sampuli za dawa za binadamu zilifuatiliwa na kuchunguzwa katika kipindi cha miaka minne zikikidhi kwa kiwango cha asilimia 96, huku dawa za mifugo zikikidhi asilimia 90.

"Matokeo haya ni kiashiria kuwa kiasi kikubwa cha dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko la Tanzania Bara zinakidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi," anasema Fimbo.

Anaeleza kwamba, mamlaka imeweka mifumo sahihi ya ufuatiliaji madhara yatokanayo na matumizi ya dawa na vifaa tiba ili aweze atambue, tathmini na kuzuia madhara yasiyovumilika kutoka kwa wananchi.

Ili kuimarisha upatikanaji taarifa hizo, hivi sasa TMDA imeanzisha mfumo wa kielektroniki ujulikanao 'ADR reporting tool' wa utoaji taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa kwa kutumia simu za mkononi au kompyuta na njia ya kutuma ujumbe wa simu.

### MAABARA

Anasema, TMDA imeimarisha shughuli za maabara kwa kuongeza vifaa vya uchunguzi, ikiwamo ufungaji wa maabara ndogo 25 zinazohamishika katika vituo vya forodha'

Fmbo anasema, katika kipindi cha miaka minne sasa, matokeo ya uchunguzi wa sampuli yanaonyesha bidhaa zilizochunguzwa zimekidhi viwango vya ubora na usalama kwa wastani wa asilimia 90.

Anaendelea: "Maabara ya uchunguzi wa dawa, imekidhi vigezo vya kimataifa na kutambuliwa rasmi na Shirika la Afya Duniani (WHO), maabara ya uchunguzi wa 'maikrobaiolojia imepata ithibati kwa kiwango cha kimataifa."

Pia, anaendelea kwamba, mwaka 2012 baada ya kukidhi viwango vya mifumo ya maabara kitaifa na kimataifa, hivi sasa mwananchi ana uhakika wa uamuzi wa mamlaka kuhusiana na ubora wa bidhaa.

Mkurugenzi anajivunia kwamba, kupitia mikoa 23 ya Tanzania Bara, programu za elimu kwa umma zimerushwa kupitia televisheni na radio za kibiashara na kijamii nchini, akifafanua namna ujumbe na matumizi sahihi ya bidhaa ulitolewa kwa wananchi.

Pia, kunatajwa kuwapo mifumo mbalimbali iliyoundwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), taarifa na takwimu za TMDA zikiwamo bidhaa na majengo yaliyosajiliwa na za wateja zimewekwa katika mfumo maalumu (IMIS), zikirahisisha utoaji huduma za vibali kwa wateja vinavyotolewa ndani ya saa 24 sasa.

"Ili kusogeza huduma za kimaabara karibu na wananchi na kupunguza gharama na usumbufu kwa wateja katika Kanda ya Ziwa, TMDA imejenga maabara kubwa na ya kisasa jijini Mwanza kuhudumia mikoa ya Kanda ya Ziwa," anasema.

### WADAU JE?

Hadi sasa inaelezwa mamlaka imeendelea kuboresha ushirikiano na taasisi nyinginezo, TMDA inashiriki kwenye mipango ya kudhibiti dawa na vifaa tiba katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Bara la Afrika (SADC).

"TMDA imetambulika kufikia ngazi ya tatu (Maturity Level 3) ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya ubora wa mfumo wa udhibiti wa dawa. Hatua hii imeifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kufikia hatua hii," anasema mkurugenzi.

Fimbo anajigamba, TMDA imekuwa mshindi wa kwanza kwa ubunifu wa mfumo wa utoaji huduma kwa wananchi katika Wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika mwaka jana na imetunukiwa Tuzo ya Ubunifu na katika Mkutano wa Umoja wa Nchi za Afrika jijini Nairobi, meaka uliopita.

"Kwa hatua hizi, TMDA imeweza kushuhudia kufikiwa kwa dira yake ya kuwa taasisi ya mfano barani Afrika katika udhibiti wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi, hivyo kuvutia nchi mbalimbali kuja kujifunza mifumo iliyopo na kwenda kuitekeleza nchini kwao.

"Baadhi ya nchi ambazo zimetuma watendaji wa taasisi zao za udhibiti kuja kujifunza mifumo ya utendaji ya TMDA ni pamoja na Zimbabwe, Rwanda, Kenya, Uganda, Ethiopia, Sudan Kusini, Botswana, Mauritius, Lesotho, Madagascar na Bangladesh," anasema.

**MAKALA**

# Mtandao wanawake na kilio cha usawa wa jinsia katika uchaguzi

**Na Daniel Eliewaha**

SUALA la wanawake katika uongozi limekuwa gumzo katika nchi mbalimbali huku mkazo ukiwa kundi hilo kuwa na nguvu sawa na wanaume katika ngazi ya uamuzi.

Katika nchi mbalimbali kwa mfano, suala hilo limekuwa likizungumzwa katika ngazi za juu za uongozi na msisitizo mkubwa umekuwa kuwawezesha wanawake kufikia asilimia 50.

Nchini Tanzania, hivi karibuni kulikuwa na kongamano juu ya jambo hilo ambapo Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi pamoja na vikundi vya wanawake na wasichana.

Katika kongamano hilo, mtandao huo ulivitaka vyama vya siasa nchini kuhakikisha vinaweka misingi wezeshi wa ushiriki kikamilifu kwa wanawake na watu wenye ulemavu katika uongozi ndani na nje ya vyama hivyo.

"Vyama vya siasa hapa nchini ni walinzi wakuu kwa wanawake na wanaume kuingia kwenye kinyang'anyiro cha siasa, kwa kuwa vina uamuzi wa mwisho wa nani aingie na nani aachwe.

Kwa hiyo ni muhimu wachukue hatua za makusudi za kuziba mapengo ya jinsia ndani ya uongozi wa vyama," hilo lilikuwa tamko katika kongamano lililofanyika kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.



Prof. Ruth Meena alikuwa mzungumzaji katika kongamano hilo.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, mwanaharakati Profesa Ruth Meena alibainisha kuwa utafiti uliofanywa hivi karibuni unaonyesha kuwa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama haukuzingatia usawa wa jinsia kwa kuwa haukufikisha asilimia 30 ya wateule wote kwenye majimbo.

"Ingawa mchakato wa uteuzi umeshapita, tunashauri vyama vihakikishe wale wanawake wachache walioteuliwa wanawezeshwa ndani ya vyama vyao ili washinde katika uchaguzi huu. Tunategemea kwamba kwenye mchakato huu, Msajili wa Vyama vya Siasa ataendelea kusimamia utekelezaji na uwajibikaji wa suala hili," alisema.

Mtandao huo wenye asasi za kiraia takriban 60 kutoka ngazi za kijamii ulimtaka Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, ambaye alihudhuria kongamano hilo, kutoa mwongozo kwa vyama hivyo ili vizingatie haki za wanawake na watu wenye ulemavu , kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2019 kifungu cha 6 A.

"Chama cha siasa kinaweza kuanzishwa na kutekeleza malengo yake ili mradi yasikinzane na misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Misingi hii ni pamoja na demokrasia, utawala bora na kutokubaguliwa kwa msingi wa jinsia," kinabainisha kifungu hicho.

Pia kifungu hicho kiliendelea kupambanua maeneo ya kuzingatia usawa wa jinsia wakati wa kutayarisha na kutekeleza sera za vyama, uteuzi wa wagombea nafasi za uongozi za uchaguzi, uchaguzi wa viongozi wa vyama na sheria ya maadili inayozongatia msingi ya usawa wa kijinsia kwenye utekelezaji wa sheria hiyo iliyopitishwa na Bunge, Septemba, mwaka jana.

Profesa Meena alimwomba Msajili kuhakikisha vyama vyote vinachukua hatua za makusudi za kujenga mazingira wezeshi ili kuwezesha makundi yote yanayoshiriki kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu ikiwa ni pamoja na wajawazito, wanawake wanaonyonyesha, watu wenye ulemavu na wazee.

Alisema ingawa mchakato wa kupata wajumbe wa viti maalum umeshakamilika, kutokana na uzoefu wa uchaguzi mkuu wa 2015, kuna baadhi ya vyama ambavyo havikupeleka kwa wakati majina ya wagombea Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), jambo lililosababisha malalamiko mengi ya uchaguzi kugubikwa na kukosa uwazi. Alivikumbusha vyama vyote kufuata utaratibu na sheria kuhusu suala hili.

"Kwenye hili tungemshauri Msajili wa Vyama vya Siasa kuongeza nguvu kwenye kusimamia utekelezaji wa msingi huu kwa kuwa ana mamlaka ya kisheria kusimamia utekelezaji wa miongozo hiyo," aliongeza Prof. Meena.

**MAENEO KIKWAZO**

Baadhi ya malalamiko ambayo kinamama wa mtandao waliyasema ma kuhusu wagombea wanawake ni pamoja na rushwa ya kawaida na rushwa ya ngono hutumika mara kwa mara na kuondoa utu wa mgombea mwanamke hivyo kuathiri mazingira yake ya ushindi.

Pili, lugha za kudhalilisha zikiwemo za kejeli, matusi, utani wa kupitiliza zimekuwa zikitolewa na ilani hiyo pia ililenga kuiambia serikali iliyopo madarakani kuwa ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha uwanja wa ushindani wa kisiasa unakuwa huru na salama kwa makundi yote, hususan wanawake ambao mara nyingi huonewa.

Vilevile ilani ililenga vyombo vya habari kutokana na uwezo wao wa kugusa mtazamo wa jamii kuhusu nafasi ya wanawake katika uongozi na maendeleo ya taifa.

Jaji Mutungi, akifunga kongamano hilo kwanza, alishukuru wanamtandao na WFT kwa kutayarisha mada mbalimbali na akaahidi atayafanyia kazi mawazo yaliyotolewa na washiriki wote.

Alisisitiza kuwa uchaguzi wa mwaka huu ili uwe mzuri na wa amani lazima haki na wajibu wa utekelezaji wa sheria zilizowekwa ufanyike.

" Ni kweli haki ni tunda la amani, lakini tusisahau vilevile kuwa kuna wajibu unaofaa kuzingatiwa wakati wa kutekeleza hiyo haki, na ni dhamira ya kutovunja sheria zilizowekwa ili uchaguzi uishe kwa amani na salama," alisema.



Wanawake wanakuwa wengi katika mikutano ya kampeni na mtaji mkubwa wa kura kwa vyama vya siasa. **PICHA: MTANDAO.**

HABARI KIMATAIFA

# Trump, Biden wachuana kwenye mdahalo

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump na mpinzani wake Joe Biden, juzi walipambana vikali katika mdahalo wa pili na wa mwisho kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mwezi unaokuja.

Mdahalo huo uliofanyika kwenye mji wa Nashville katika jimbo la kusini la Tennessse, uliwakutanisha wagombea hao wawili baada ya ule wa mwanzo kushindwa kutoa mshindi.

Kama ilivyotarajiwa wagombea wote wawili, Trump anayewania muhula wa pili kupitia Republican na Biden kutoka chama cha Democratic, walilumbana kuhusu uchumi na ugonjwa wa Covid-19.

Biden ambaye alikuwa makamu wa rais wa Marekani wakati wa utawala wa Barack Obama, alimshutumu Trump kuwa mtu asiyefaa tena kuwa rais wa nchi hiyo kutokana na vifo vya Wamarekani zaidi ya 200,000 vilivyotokana na virusi vya corona.

Alisema Trump hana mkakati wowote katika kudhibiti maambukizi ya virusi, hivyo ni muhimu kuachana naye.

Hata hivyo, Rais Trump alimjibu kwa kueleza Wamarekani wanapaswa kutoka nje na kufanya kazi.

Mdahalo wa juzi uliofanyika katika hali ya kuheshimiana, tofauti na ule wa kwanza ambao wagombea hao walirushiana maneno makali.

Rais Trump, alidai chanjo dhidi ya virusi vya corona inakaribia kupatikana na kumshutumua Biden kuhatarisha taifa hilo kutokana na uhusiano wake na mtoto wake nchini Ukraine.

Alidai familia ya Biden ilijipatia mamilioni ya dola kutoka Ukraine, pamoja na kufanya vitendo visivyo vya maadili nchini China na Ukraine.

Trump alimtuhumu Biden kuwa alipokea fedha kutoka nchi ya Urusi.

Biden alipinga vikali madai hayo hayo na kuitetea familia yake kuwa haikuwahi kupokea hata senti moja kutoka nchi ya kigeni.

Alisema madai ya Trump, ni kujaribu kuwavuruga Wamarekani ambao wanataka kiongozi huyo ameweka wazi mrejesho wa ulipaji kodi kwa kipindi cha miaka 22.

Biden alimtaka Trump aonyeshe marejesho yake ya kodi badala ya kuwapakazia wenzake maneno yasiyo na ushahidi.


Kwa mara nyingine, Trump alijitetea kuhusu madai ya kuwa na akiba ya benki nchini China, alisema fedha hizo ni za mwaka 2010 wakati alipokuwa mfanyabiashara.

Kuhusu madai ya kuingiliwa kwa uchaguzi wa Marekani na mataifa ya nje, Biden alisema ameweka wazi kuwa nchi yoyote, bila kujali ni ya nani, itakapobainika kuingilia kati uchaguzi wa Marekani, basi, italipa gharama kubwa.

Mdahalo huo ulioonekana moja kwa moja kwenye televisheni ulikuwa ni fursa ya mwisho kwa Trump kuwasihi wapiga kura kumuunga mkono na kumchagua kwa mara nyingine.

Kura za maoni zinaonyesha Rais Trump, yuko nyuma ya Biden, ingawa mchuano ni mkali katika baadhi ya majimbo ambayo yana uwezo mkubwa wa kubadili matokeo.

**BBC**



Rais wa Marekani, Donald Trump, akijibu maswali kutoka kwa mpinzani wake Joe Biden, kutoka chama cha Democratic, wakati wa mdahalo wa mwisho uliofanyika usiku wa juzi. **(PICHA: AP)**

# Korea yatahadharisha upepo wenye vumbi

**PYONGYANG, Kosea Kaskazini**

KOREA ya Kaskazini imetahadharisha raia wake kubaki ndani ya nyumba zao kutokana na hofu ya vumbi la njano linalopepea kutoka China, linaweza kubeba virusi vya corona.

Mitaa ya mji mkuu Pyongyang iliripotiwa kuwa mitupu siku ya Alhamisi, baada ya vyombo vya habari kutoa tahadhari hiyo.

Nchi hiyo ambayo ilidai haina maambukizi ya virusi hivyo, lakini tangu mwezi Januari imekuwa kwenye hali ya tahadhari pamoja na kuchukua hatua ya kufunga mipaka.

Hata hivyo, hakuna uthibitishi wa kisayansi kuwa mawingu hayo ya vumbi ya msimu wa vumbi yanaweza kubeba virusi hivyo.

Tahadhari hiyo haikuchukuliwa na Korea Kaskazini pekee, kulingana na BBC, hata nchi ya Turkumenistan, pia iliwataka raia wake kuvaa barakoa ikidai uwepo wa virusi kwenye vumbi.

Televisheni Korea Kaskazini, (KCTV) ilitangaza katika kipengele cha hali ya hewa siku ya Jumatano, kuwa kutakuwa na vumbi la njano siku inayofuata na kupiga marufuku watu kutoka nje na kufanya kazi.

Vumbi lenye rangi ya njano linatokana na mchanga kutoka jangwa la Mongolia na China na husafirishwa hadi Korea ya Kaskazini na Kusini katika msimu wa mwaka.

Ubalozi wa Urusi uliopo Pyongyang, ulisema katika ukurasa wake wa Facebook kuwa wizara ya mambo ya nje ya Korea Kaskazini, iliionya pamoja na ofisi nyingine za kidiplomasia na mashirika ya kimataifa nchini humo, kuhusu upepo wenye vumbi na iliwataka wageni wote kubaki nyumbani na kufunga madirisha yao.

**BBC**

# Ndege za Israel zashambulia Gaza

**TEL AVIV, Israel**

ISRAEL imetangaza kufanya mashambulizi ya anga usiku wa kuamkia jana katika Ukanda wa Gaza, baada ya wanamgambo wa Kipalestina kurusha roketi mbili.

Hata hivyo, taarifa kutoka jeshi la nchi hiyo, haikusema chochote kuhusu vifo au athari zilizotokea katika pande zote.

Jeshi hilo lilisema ndege zake za kivita na nyenzo nyingine za kivita zilishambulia eneo linalodaiwa kutumika kutengenezea silaha na miundombinu ya chini ya ardhi ya kundi la Hamas, ambalo linatawala eneo la Gaza.

Israel na Hamas wanashambuliana kila mara tangu kundi hilo lenye itikadi kali za kiislamu kufanikiwa kulidhibiti eneo la Gaza.

**DW**

# Uingereza yakiri kutegemeana biashara na Umoja wa Ulaya

**LONDON, Uingereza**

NAIBU Waziri wa Fedha wa Uingereza, Stephen Barclay, amesema mpango wa biashara wa baada ya Uingereza kujiondoa katika Umoja wa Ulaya (Brexit) ni matakwa ya pande zote.

Hata hivyo, alisema unaweza kufanikiwa, endapo Umoja huo utaheshimu uhuru wa mipaka katika sekta ya uvuvi.

Akizungumza na shirika la utangazaji la Sky News, waziri huyo alisema mkataba unapaswa kuakisi ukweli wa taifa hilo katika umoja huo kwenye kupata haki ya kudhibiti.

Mjadala kuhusu mipaka ya uvuvi, ulikuwa muhimu katika kipindi cha majadiliano ya Brexit.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**SHAMBA L INAUZWA LIPO KIBAHA KONGOWE** Shamba linauzwa lenye ekari 10 Tsh 25,000,000 lipo kibaha kongowe umbali kutoka barabarani hadi shamba KM 9 Kwa mawasiliano zaidi 0754826580.

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWASAM MOHAMEDI AMANI** anatangaza kupotelew kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0582/0022,** kilichotolewa na shule ya secondary **UNUNIO ISLAMIC** mwaka 2016,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MWK/LF123/2020**

115957802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 89 YA 2020**

**GWAKISA MWAKALOBO MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**RHODA ADAM MWAKALOBO MAREHEMU**

**Kwa, Yeyote anayehusika maslahi**

Kwakua mdai ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwahiyo mtu yeyote mwenye maslahi katika maombi ya mirathi tajwa hapo juu anapaswa akuweka pingamizi na kuhudhuria katika mahakama hii ya wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 23 mwezi 11 mwaka 2020 saa mbili (2;00) kamili asubuhi. Kwakua siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa akuja na vielelezo vyote vinanvyohusiana na maombi ya mirathi hii.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama leo tarehe 22 mwezi 10 mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI

115957202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**

**SHAURI NA. 341 LA 2020**

**BONIFACE IDINDILI..............................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **AZIZ JUMA**
2. **HALIMA ADAM JUMA ..................................WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: AZIZ JUMA NA HALIMA ADAM JUMA**

Mnafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 26/10/2020 katika Chumba cha Baraza, Barabara ya Posta. Jengo liko Mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.
Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyinyi kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo 25/09/2020.

MAYEYE S. M.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

115957502

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA AT MWANZA**

**PROBATE AND ADMINISTRATE CAUSE NO 05/OF 2020**

**IN THE MATTER OF THE PROBATE OF THE LATE BARAKA LEONARD NAFARI**

**IN THE MATTER OF THE PROBATE AND ADMINISTRATION OF ESTATE ACT**
**AND**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BARAKA LEONARD NAFARI**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR APPOINTMENT OF EXECUTOR OF THE ESTATE OF BARAKA LEONARD NAFARI BY NAOMI PAULO CHABANDI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th of november, 2020.
Dated at mwanza this 21 of october,2020.

RESIDENT MAGISTRATE
MWANZA

COPY TO
PETER H.KIPFUMU ( ADVOCATE)
BOX 44
MWANZA

115957402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;326/2020**

**Ombi la BETHA GIDION NGUKU ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ISACK YOTHAM ILOMO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/10/2020.

Sahihi ya Hakimu

115957902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA MJINI WILAYA YA MOROGORO**

**MADAI NAMBARI...120..2020**

**Mdai; ELIANA SIMON KAGALI**

**Anamdai**

**mdaiwa; SADIQ SIMON MASINI**

**Kwa; SADIQ SIMON MASINI**

Kwakuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai Yake/Yao Kwamba/Eleza Hapa habari ya madai; Madai ya TARAKA kwahiyo anahitajiwa/Mnahitajiwa ktk Mahakama hii siku ya tarehe 27/10/2020 Saa 8:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo,kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta Mashahidi wako/wetu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea ktk shauri hilo.
Angalia kama hukuudhuria /Hamkuhudhulia siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha Kama umepokea /Mmepokea Kuitwa shaurini hii,Itaweza kutoa hukumu kuwa Umeshindwa/Mmeshindwa.Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 19/10/2020.

115958002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 157/2020.**

**Ombi la KURWA MBWANA MAPEE kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu EDWARD TUNGU KAPELLA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 12/11/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 23/2020.

Sahihi ya Hakimu

115958102

---

## KUPOTOLEWA KWA KADI YA GARI

**FARIDA GULAM HUSSEIN**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya Toyota **MARK X** yenye namba za usajili **T 986 DHE,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/KIJ/RB/757697/2020**

115958502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;324/2020**

**Ombi la RENALDA ANTHONY KESSY ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LIVINGSTONE A.ELISA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/10/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115958402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA KILOSA**

**KESI YA RUFAA YA MADAI NO: 23/2020.**

**BENNY MAKUNDI..............................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MJIBU MAOMBI**
**BENNY E. HAULE t/a**
**B.S.C FAST FOOD AND TAKE AWAY**

**BENNY E.HAULE t/a B.S.C FAST FOOD AND TAKE AWAY,**

Unaamriwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe binafsi au wakili wako, Mnamo tarehe 04/11/2020.Kwenye shauri la Madai na.23/2020. Hivyo unatakiwa kufika bila ya kukosa tarehe hiyo.

Hati hii imetolewa Leo tarehe 20/10/2020 mbele ya Mahakama ya Wilaya KILOSA.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KILOSA

115958702

---

## KUPOTOLEWA KWA KADI YA GARI

**SEAWAYS TANZANIA CORPORATION** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **CRANE FORK LIFT** Yenye namba za usajili **T 531 DMZ ,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/MAG/RB/757494 /2020**

115958602

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

**Nipashe** MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-**35**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

ALIREJEA chumbani na kwenda kumuamsha mpenzi wake Shani.

"Ilikuwa uhame wiki ijayo hapa, lakini haiwezekani, leo hii hii utahama na kuhamia kwangu. Hapa si salama tena."

Sauti ya Eddy ilipenya masikioni mwa Shani. Ni kweli aliingiwa na woga, ingawa hakujua vibaka wale nia yao ilikuwa ni kuiba nini mle ndani.

Ni Eddy tu aliyejua kuwa kama siku ile asingekwenda nyumbani kwa Shani, basi asingemuona tena maishani.

Mwili ulimsisimka. "Sijui ingekuwaje?" Alijiuliza. Tangu alipoonana na Shani alitokea kumpenda na hakutaka kitu chochote kile kitokee cha kumtenganisha naye.

Ni mwanamke ambaye amembadilisha kuwa mwanaume wa kwenda kustarehe kwenye mahoteli na mabaa na wanawake warembo wa kila aina, hadi kuwa mwanaume mwenye kupenda na kujali.

Urembo wa msichana yule mdogo tu wa miaka 23, pamoja na misukosuko ya hatari anayopitia bila yeye kujua sababu yake, ilimfanya Eddy kumuonea huruma, ikiwemo kuzidi kumpenda na kuwa naye karibu.

Na ndiyo maana awali alimwambia atakuwa akija nyumbani kwake kumchukua, kumpeleka na kumrudisha nyumbani kila asubuhi na jioni, tena akitumia gari lake, badala ya gari la msichana huyo ambalo aliona watesi wake watakuwa wanalifahamu na kulifuatilia.

Alichofanya Eddy ni kulichukua Land Cruiser la Shani na kulificha nyumbani kwake Kijitonyama.

Na hii ni baada ya kugundua kuwa kuna watu wanatafuta kumuua kwa sumu ambayo angeila kwenye chakula siku ile ABC Hotel kama yeye asingegundua hilo.

Leo kuna watu wamevamia nyumbani kwake. "Nadhani lengo ni lile lile kumuua." Alijiambia.

"Ni kweli mpenzi. Kwa hali hii mimi siwezi kukaa hapa na kulala peke yangu." Alijibu kwa sauti ya upole.

"Ningeweza kusema mimi nikae hapa na wewe, kwa sababu wote hatutokuwa salama, nadhani itakuwa si vizuri sana. Twende kwangu ukakae kwa usalama zaidi hapo tutapokuwa na uhakika wa usalama wetu."

Ving'ora vilisikika na magari matatu yaliwasili hapo. Eddy alitoka kwanza na kwenda kuongea nao nje. Alipoingia aliwaruhusu baadhi ya watu kuingia ndani. Kuna waliochukua maiti ya aliouawa na kuondoka nayo kwa gari la wagonjwa. Jamaa aliyepona alichukuliwa na gari lingine, huku watu wanne wakibaki kulinda nyumba.




**Umekuwa sababu ya mimi kuchanua upya kwenye maisha yangu. Pamoja na mali nilizoachiwa na wazazi wangu, lakini sikufikiria kama ningepata furaha tena kama hii maishani kwangu. Nakupenda sana Eddy.**

"Sherry hawa ni walinzi ambao watakuwa wakiilinda nyumba hii muda wote ambao hatupo. Sasa na sisi naona tujiandae kuondoka, kusanya ambacho unachoweza kukitaka kutumia kuondoke."

Hii ya walinzi ilishangaza kidogo Shani, lakini kutokana na mambo yalivyokuwa, hakutaka kujiuliza sana zaidi ya kujiandaa

"Haya Sherry ngoja nijiandae."

*******************************

Ushauri ambao Eddy alimpatia Shani ni kuomba likizo ya mwezi mmoja ya bila malipo ofisini kwake. Shani aliutekeleza. Aliambiwa kuwa anahitaji kuwa karibu na yeye zaidi. Hiyo ilikuwa ni baada ya msichana huyo kuhamia nyumbani kwa Eddy.

Eddy alikuwa ameua ndege wawili kwa jiwe moja. Alipata muda wa kukaa zaidi na kumuelewa msichana huyo.

Alipata muda wa kucheza naye. Kula naye, kudekezana, na kila aina ya wapenzi wanaopendana kwa dhati wanavyofanyiana.

Kila mmoja alipata kumfahamu mwenzie vizuri zaidi. Kila mmoja alimfurahia mwenzie. Kila mmoja aliwaza kwa nini asingemfahamu miaka mingi nyuma.

"Unajua nilianza kukupenda tangu siku ya kwanza nilipokuona, lakini sikutegemea kabisa utakuwa mwanamke wa maisha yangu. Sikutegemea kuwa leo ungekuwa hapa. Ungekuwa na mimi hapa. Najihisi mwenye bahati kubwa sana." Eddy alinong'ona huku akimpapasa mabegani.

Shani alikaa kimya kama mtu anayewaza kitu. "Nikwambie kitu Eddy?" Ghafla aliibuka.

"Niambie mpenzi wangu." Aliitikia Eddy mkono wake ukiendelea na ziara ya kupapasa mwili wa mrembo wake.

"Kila mmea humea na kuchakua pale tu linapopata maji na mbolea." Ni maneno yaliyotoka kwenye kinywa cha Shani kwa utulivu wa hali ya juu, yaliyoingia kwenye masikio ya Eddy mpaka kwenye moyo wake.

"Na kama litatambaa, basi hutambaa kutokana na mhimili uliowekwa kwa ajili ya ua hilo. Na ndivyo ulivyo kwangu. Umekuwa sababu ya mimi kuchanua upya kwenye maisha yangu. Pamoja na mali nilizoachiwa na wazazi wangu, lakini sikufikiria kama ningepata furaha tena kama hii maishani kwangu. Nakupenda sana Eddy." Alinong'ona huku machozi yakimtoka.

Ni mtoto wa kike. Tena mwenye umri mdogo tu ambaye hakuonja sana malezi ya mama yake mzazi. Alifariki akiwa bado mdogo. Alilelewa na mahausigeli na baadhi ya ndugu wa baba yake.

Kifo cha baba yake kilizidi kumtia simanzi na kumuongezea machungu. Lakini tangu alipokutana na mtu mmoja anaitwa Eddy alihisi kuwa huenda ni mtu ambaye alikuwa anatamani siku moja kuwa naye.

Kadri siku zilivyozidi kwenda, alizidi kumpenda na kumuamini. Kwa sasa ameuachia moyo wake kwa Eddy.

Hakupata kudeka kwa mama yake. Sasa anadeka kwa Eddy.

"Jamani natamani mimi ningekuwa mkeo, natamani kudeka kwa mtu ninayempenda, lakini sijui kama nitapata nafasi hiyo." Alisema akiwa amejilaza kwenye miguu yake mpenzi wake.

"Kwani hapa wewe unafanyaje? Si unadeka tu hapa. Nakupa nafasi ya kudeka kuanzia sasa na kuendelea huko mbele kama Mungu akitujaalia."

Wapenzi hao wawili walikumbatiana. Damu zilizokuwa kwenye miili yao zilitengeneza joto ambalo kila mmoja alilihisi kwenye mwili wa mwenzake. Mapigo yao ya moyo yakaongezeka. Mikono yao ikaendelea kufanya ziara kwenye miili kila mmoja hapa na pale. Kila mmoja alisijikia raha kama anapaa angani.

***************************

"Umesema unaitwa George Kupila si ndiyo?"

"Sawa Kabisa."

"Okay, mimi sina mengi sana. Ila ningependa nikuulize swali moja tu."

George hakujibu kitu, badala yake sura ilionekana kutaka swali liulizwe.

"Unamfahamu Timo?"

"Timo yupi?"

"Kijana mmoja msela hivi ambaye alipewa kazi ya kumuua Fikiri."

Kwa mbali Eddy alihisi mshtuko kwenye moyo wa George.

Macho yalimtoka pima na mapigo ya moyo yakaongezeka.

Eddy alikuwa na uzoefu na mambo hayo, hivyo aliona hali isiyo ya kawaida kwenye uso wa George.

Awali aliambiwa aripoti kwenye Kituo Kikuu cha Polisi, baada ya kuambiwa gari lake lilikuwa na makosa ya usalama barabarani. Haikuwa hivyo. Eddy aliamuru hivyo, baada ya kubainika kuwa gari hilo ndilo lililokuwa na mtu ambaye alikuwa na Timo, muda mfupi tu kabla ya kifo cha Fikiri.

Timo ambaye yupo kizuizini alieleza yote baada ya kupata kibano.

George ambaye ndiye mmiliki wa gari alipofika hapo kituoni, askari alimpigia simu Eddy ambaye alimtuma mmoja wa wafanyakazi wa ofisi yake kwenda kumchukua kumpeleka kwenye ofisini mwake.

"Timo huyo huyo unayemfahamu wewe."

"Simjui mimi huyo."

"Sawa, hilo tutalijua." Eddy alinyanyua simu na kumwita mmoja wa wafanyakazi.

"Mlete yule jamaa yetu tuliomuweka ndani majuzi."

Baada ya dakika mbili mlango ulifungiliwa na mfanyakazi huyo aliingia na Timo.

George alionekana kupatwa na mshtuko alipomuona.

"Timo, umekaa ndani inakaribia wiki sasa. Sasa kama unataka kwenda uraiani, hebu niambie huyu unamfahamu?"

"Ndiyo."

"Ni nani?"

"Jina simjui, lakini huyu ndiye aliyenipa pesa na kunituma nimuue Fikiri."

"Una uhakika kuwa ni huyu?"

"Nina uhakika kwa sababu hatukuonana siku moja. Siku ya kwanza tulionana na siku ya pili pia tulionana, siwezi kumpotea."

"Unasikia bwana George, huyu atakuwa ndiye shahidi kwenye kesi yako tutakapokwenda mahakamni, kwa hiyo sina shaka na hili. Swali langu la pili ni kwa nini ulitaka Fikiri auawe?"

ITAENDELEA JUMAMOSI

# MOURINHO ASIFIA WACHEZAJI WAKE




**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesifia nguvu ya Tottenham baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya LASK kwenye mchezo wa Ligi ya Europa, juzi Alhamisi.

Wachezaji watatu tu, Davinson Sanchez, Ben Davies na Sergio Reguilon, waliendelea kucheza kwenye nafasi zao kutoka kikosi kilichotoka sare ya 3-3 na West Ham Jumapili iliyopita kwenye Ligi Kuu England.

Mounrinho aliamua kukibadilisha kikosi chake kwenye mchezo huo na akafanikiwa kupata matokeo hayo muhimu kwenye mchezo huo uliopigwa jijini London.

"Nina furaha na kikosi," alisema Mourinho akiiambia BT Sport mara baada ya mchezo huo.

"Tunawaamini wengine kwa sababu wanafanya kazi kubwa na huwa wapo tayari kucheza wakati wowote.

"Kwa kawaida sio kitu kibaya kubadili wachezaji pale unapoona mambo hayaendi sawa, na kwa hakika kila kitu kilikwenda sawa.

"Vijana wangu walicheza kwa kujituma tangu dakika ya kwanza na hakika tulistahili ushindi huu."

Wachezaji kama Son Heung-min, Dele Alli na Giovani Lo Celso waliingiza kwenye mchezo huo wakitokea benchi.

# Guardiola atoa neno kwa Virgil Van Dijk

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amemtumia ujumbe wa kumfariji mlinzi wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk baada ya kuumia goti wikiendi iliyopita na kufanyiwa upasuaji.

Van Dijk huenda akakosa sehemu kubwa ya msimu huu baada ya kugongana na golikipa wa Everton, Jordan Pickford, katika mchezo baina ya timu hiyo pale kwenye Uwanja wa Goodison Park ambao ulimalizika kwa sare ya kufungana mabao 2-2.

Wakati hilo likionekana kuwa pigo kubwa kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England, lakini Guardiola haamini kama hilo litakuwa tatizo kubwa kwa miamba hiyo ya Anfield.

City wenyewe msimu uliopita walikumbana na janga kama hilo wakati walipompoteza beki wao wa kati, Aymeric Laporte kwa muda wa miezi minne kutokana na kuumia goti.

Jambo ambalo Guardiola anaona kwamba, Liverpool bado itakuwa na nafasi ya kufanya vizuri kwenye ligi hiyo kwa sababu ina wachezaji wengi.

" Sitaki kuzungumzia namna Liverpool watakavyoathirika, kwani Jurgen ndiye mwenye mamlaka ya kuzungumzia hilo," alisema Guardiola akinukuliwa na Sky Sport.

"Lakini naona hilo halitakuwa tatizo kuubwa kwao, kwani hata sisi tulikuwa bila beki wetu muhimu Laporte kwa miezi minne, naamini Liverpool watalikabili vizuri hilo."





# *Arteta: Ozil atakiwa ajilaumu mwenyewe*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amejibu, Mesut Ozil kwa kusema anatakiwa ajilaumu yeye mwenyewe kwa kushindwa kutimiza majukumu yake.

Ozil ameachwa kwenye kikosi cha Arsenal kinachoshiriki Ligi Kuu England na Ligi ya Europa kwa msimu huu.

Arteta akijibu tuhuma za Ozil, amesema ameleta vita ndani ya klabu ambayo haina ukweli kwa kulituhumu benchi la ufundi na amekosa heshima na kutambua thamani yake.

Ozil juzi alitoa taarifa ya kuachwa kwake katika mtandao kwa kusema hajatendewa haki na ataendelea kujifua kwenye kwenye mazoezi.

Lakini Arteta alisisitiza kuwa Ozil hana mtu wa kumlaumu zaidi ya yeye mwenyewe, akimaanisha kuwa nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani alishacheza mechi ya mwisho ya klabu hiyo.

"Kitu kinachotokea kwa Ozil kwa sasa si kitu kipya," alisema Arteta akinukuliwa na BBC Sport.

"Hali niliyomkuta nayo wakati najiunga na klabu hii ilikuwa ngumu, mambo haya yamekuwa yakitokea kwa miaka nane sasa.

"Kazi yangu ni kuimarisha viwango vya wachezaji kuleta timu bora uwanjani, lakini kwa sasa nahisi kama nimeshindwa kwa upande wake, kwani nilimtaka Ozil mwenye kiwango bora."

## HABARI MICHEZO

# Lippi: Nimemaliza kila kitu kwenye ukocha

**ROME,** Italia

KOCHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya Italia, Juventus na mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2006, Marcello Lippi amesema "ameshamaliza kila kitu" kwenye kazi ya ukocha.

Lippi amekuwa hana kazi tangu alipojiuzulu kuinoa Timu ya Taifa ya China Novemba, mwaka jana baada ya kipigo kutoka kwa Syria kwenye mbio za kuwania kufuzu michuano ya Kombe la Dunia mwaka, 2022 akiwa amekaa kwenye nafasi hiyo kwa miezi sita tu.

Lippi mwenye umri wa miaka 72 alibeba Kombe la Dunia na Italia, taji la Serie A akiwa na Juventus na Kombe la Ligi Kuu China akiwa na Guangzhou Evergrande na sasa amesema hana mpango wa kurudi kwenye kazi hiyo.

"Kwa sasa nimemaliza kila kitu kwenye ukocha," alisema Lippi akiiambia redio Sportiva. "Kwa sasa inatosha."

"Pengine naweza kutumika kwa nafasi nyingine, ngoja tuone. Lakini sio tena kwenye kazi ya ukocha."

Baada ya kuzinoa Atalanta na Napoli, Lippi alichukua mikoba ya kuinoa Juventus mwaka 1994, akiwawezesha Bianconeri kutwaa mara tatu taji la Serie A na taji la mwisho kwa klabu hiyo la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 1995-96.

Baada ya kuondoka Juventus mwaka 2004 akiwa pia ameifundisha Inter Milan mwaka mmoja, Lippi aliisaidia Italia kubeba Kombe la Dunia mwaka 2006 na aliteuliwa tena kuwa kocha wa Azzurri hao mwaka 2008.

Nchini China, Lippi alijiunga na Guangzhou Evergrande mwaka 2012 na kutwaa mataji matatu ya Ligi Kuu na lile la Ligi ya Mabingwa Asia.






# FERDINAND AKUNWA NA RASHFORD

**LONDON,** England

KIWANGO cha Marcus Rashford alichokionyesha kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Manchester United ikiibuka na ushindi dhidi ya PSG kimemkuna Rio Ferdinand.

United ilipata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi dhidi ya PSG jijini Paris, Jumatano.

Na beki wa zamani wa mashetani wekundu hao Ferdinand amesisitiza mchezaji huyo atakuja ataendelea kuwa na kiwango cha kuvutia zaidi siku za usoni.

Rashford ndiye aliyefunga bao la ushindi la United katika mchezo huo na Ferdinand amesisitiza kwa sasa bado anapikwa na wakati utakapofikia atazidi kuonyesha makali zaidi ya haya.

"Anaonekana kufunga mabao magumu sana, jambo ambalo hata Wayne Rooney katika siku zake za kwanza hakuwa anafanya hivyo," alisema Ferdinand akinukuliwa na Sky Sport.

"Ikiwa ataendelea na tabia hii ya kufunga kwenye mazingira magumu naamini atakuwa moto wa kuotea mbali kwa kuwa atakuwa na uwezo mkubwa wa kufunga mabao rahisi.

"Anaijua nafasi yake uwanjani na mara nyingi huwa na kitu kikubwa ni tabia yake ya anapopata nafasi moja kwa kuitumia kwa usahihi."

# *Lampard afunguka atakavyomtumia Silva*

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesema atamtumia mlinzi wake mkongwe, Thiago Silva kwa tahadhari kubwa nyota huyo wa Brazil kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Sevilla.

Chelsea iliingia kwenye mchezo huo ikionekana kuwa na matatizo kwenye safu yake ya ulinzi, baada ya kulazimishwa sare na Southampton dakika za mwisho kwenye Ligi Kuu England.

Silva alirudi kikosini na kuonyesha uzoefu kwa kutoruhusu bao kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Na sasa Lampard anaona Silva mwenye umri wa miaka 36, anatakiwa kutumiwa kwa tahadhari kubwa kutokana na umri wake.

"Silva hatacheza katika kila mchezo, ingawa kwenye mechi anayokuwapo yeye timu inakuwa tofauti," alisema Lampard akinukuliwa na Sky Sport.

"Nilizungumza kuhusu ubora na uzoefu kabla ya mchezo na bahati nzuri amefanya vyote na alikuwa na mchezo mzuri.

"Ana uwezo mkubwa hasa katika suala la kutoruhusu kufungwa. Zaidi ya msimu, nitajaribu kumlinda na uzuri ni kwamba nina ukaribu naye licha ya kutumia mkalimani."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ZIDANE AKALIA KUTI KAVU REAL MADRID

Mfaransa huyo amepewa mechi mbili za kuamua hatima yake ndani ya kikosi hicho...

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anaweza kufukuzwa kama hatapata matokeo mazuri kwa mechi mbili zijazo, kwa mujibu wa gazeti la L'Equipe.

**Msimu uliopita, Zidane aliiwezesha Real Madrid kutwaa taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kuwapiku wapinzani wao wakubwa, Barcelona.**

Lakini sasa kikosi hicho cha Zidane msimu huu wa 2020-21 kimeanza kwa kusuasua kwenye Ligi Kuu Hispania na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Madrid imeripotiwa ipo tayari kuachana na kocha wake huyo kama timu hiyo itaendelea kupata matokeo yasiyoridhisha katika mechi mbili zijazo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mabosi wa Madrid watafikia uamuzi wa kuachana na Zidane katika mechi hizo mbili zijazo, kama atashindwa kupata matokeo mazuri.

Zidane amekuwa kwenye presha kubwa baada ya Madrid kufungwa mechi mbili mfululizo, akianza kwenye LaLiga kwa kufungwa 1-0 na timu iliyopanda daraja msimu huu ya Cadiz.

Halafu akakumbana na kichapo kwenye mhezo wa kwanza wa makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati ilipochezea kichapo cha mabao 3-2 kutoka kwa Shakhtar Donetsk.

Raia huyo wa Ufaransa, hiki ni kipindi chake cha pili kuinoa klabu hiyo yenye maskani yake makao makuu yapo katika mji wa Madrid, kwa sasa inakabiliwa na mchezo wa El Clasico dhidi ya wapinzani wao Barcelona, leo Jumamosi.

Na baada ya hapo atakuwa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Monchengladbach inayoshiriki Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Kwa kipindi ambacho ameinoa Madrid, Zidane ameiongoza Los Blancos hiyo kushinda taji la LaLiga mara mbili na mataji matatu la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO, RAUL VITANI

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino na Raul wanapewa nafasi kubwa ya kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane kama atafukuzwa kuinoa Real Madrid. ***(AS)***

### PEP KUMSHAWISHI GRACIA

KOCHA wa Manchester City, Guardiola ana matumaini kuwa anaweza "kumshawishi" mlinzi wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, kuongeza mkataba wake. ***(Independent)***

### OZIL ANUKIA MAREKANI

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil anaweza kuhamia katika Ligi Kuu Marekani (MLS), baada ya Klabu ya DC United kuonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32. ***(Sun)***

### MALEN KUREJEA ARSENAL

ARSENAL wanaangalia uwezekano wa kumsajili, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 21, kutoka klabu ya PSV Eindhoven, ikiwa ni miaka mitatu baada ya kumuuza mshambuliaji huyo wa Uholanzi kwa pauni 540,000. ***(Soccernews, via Star)***

### EVERTON ILIBAHATIKA

IMEBAINIKA mkataba wa Everton wa kumsajili Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 23, kutoka Sheffield United mwaka 2016 ulikuwa "wa bei ya chini" kuliko ilivyoripotiwa kwamba, alisainiwa kwa malipo ya pauni milioni 1.5, kwa mujibu wa kocha wa timu ya vijana ya Toffees hao, David Unsworth. ***(Sky Sports, via Mail)***

### SPURS ILIMSHUSHA RODON

KLABU ya Tottenham Hotspur walishusha bei ya mlinzi wa Wales, Joe Rodon mwenye umri wa miaka 23 kwa pauni milioni tano, tofauti na kiasi kilichokuwa kinatakiwa na Swansea na hivyo usajili wake kushindikana. ***(Football Insider)***

### KABAK ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanaelekeza nguvu zao kumsajili mlinzi wa Schalke, Ozan Kabak mwenye umri wa miaka 20, ili kuziba pengo la Virgil van Dijk mwenye miaka 29, ambaye ni majeruhi. ***(Sport Media Set, via Sport Witness)***

### PIQUE ALIIBEBA BARCA

MLINZI wa Barcelona, Gerard Pique mwenye umri wa miaka 33, alikubali kupunguza mshahara wake kwa asilimia 50 kwa kipindi cha msimu uliopita kabla ya kufikia mwisho, kwa sababu ya athari za mlipuko wa corona. ***(Sport)***

### BESIC ASUBIRI JANUARI

KIUNGO wa kati wa Everton, Muhamed Besic, ambaye ana umri wa miaka 28, hatalazimisha kuondoka na kwenda Ureno anakowaniwa kipindi hiki, hadi wakati wa dirisha la Januari mwakani. Ureno bado haijafunga dirisha la usajili. ***(Liverpool Echo)***

### REGUILON AMTAJA MOURINHO

MLINZI wa Hispania, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 23, amesema kocha wa zamani wa Real Madrid, Jose Mourinho ndiye aliyemshawishi kuhamia Tottenham. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

## Makocha Shinyanga kuendeleza vipaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WALIMU 40 wa Shule za Msingi mbalimbali mkoani hapa wamehitimu mafunzo ya ukocha wa mpira wa miguu wa ngazi ya chini yaliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Mgeni rasmi katika ufungaji wa mafunzo hayo, Ofisa Elimu wa Shule za Sekondari Manispaa ya Shinyanga, Lucas Mzungu, alimpongeza Rais wa TFF, Wallace Karia, kwa kuanzisha programu hiyo ambayo itakuwa ni chachu ya kupata wachezaji ambao watainua soka la hapa nchini.

Mzungu alisema kupitia makocha hao, anaamini watapatikana wachezaji wengi wa kulipwa ambao watasaidia kulitangaza jina la Tanzania.

Katibu wa Chama cha Soka mkoa wa Shinyanga (SHIREFA), Stephen Mihambo, alisema wamefurahishwa na mafunzo hayo, ambayo pia yatasaidia kuinua kiwango cha wachezaji kwa kuwapa elimu kuanzia ngazi ya chini.

Ruth Mgombele, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo alisema kwa niaba ya wenzake watajipanga kuyafanyia kazi kwa vitendi ili kufikia malengo ya shirikisho.

Mgombele alisema Tanzania ina wachezaji wenye vipaji lakini wamekosa makocha wa kuwatambua jambo ambalo wao watakwenda kulifanya.

## Biashara yaipigia hesabu Polisi TZ

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kupoteza mchezo uliopita wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amewataka wachezaji wake kusahau yaliyopita na sasa kuifikiria Polisi Tanzania.

Maafande hao wanatarajia kuwakaribisha Biashara United katika mchezo wa Ligi Kuu raundi ya saba utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha.

Baraza alisema tayari kikosi chake kimeshawasili Arusha na wanaendelea na mazoezi ili kuhakikisha wanaondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo.

Hata hivyo Baraza alisema katika mechi ya kesho atamkosa mchezaji wake, Omary Banda ambaye anasumbuliwa na maumivu ya nyama za paja.

"Tulicheza vibaya sana mechi dhidi ya Coastal Union, timu ilishindwa kufuata maelekezo, makosa ambayo niliyaona katika mchezo huo nimeendelea kuyafanyia kazi yasijitokeze tena katika mchezo unaofuata," alisema Baraza.

Aliongeza haihofii Polisi Tanzania licha ya kuwa na rekodi nzuri na kusisitiza kila mchezo watakaocheza kwao ni sawa na fainali.

Polisi Tanzania itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 na Yanga wakati Biashara United ilichapwa magoli 3-0 na Coastal Union.

# JULIO AMWITA MTOTO WAKE KUCHEZA CECAFA

**Saada Akida na Nyangasa,** TUDARCo

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), Jamhuri Kihwelo 'Julio', ameita nyota 52 kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), akiwamo mtoto wake, Super Julio Junior, anayecheza soka la kulipwa katika klabu ya ATM iliyoko Ubelgiji.

**Mashindano hayo ya CECAFA yamepangwa kufanyika kuanzia Novemba 20 hadi Desemba 10, mwaka huu jijini Arusha.**

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana, Julio alisema wachezaji 46 wanacheza katika ligi za ndani na atawafanyia mchujo na kubakia na nyota 24 ambao wataungana na wenzao sita wanaocheza soka la kulipwa.

Julio alisema kikosi cha mwisho kitakachokuwa na wachezaji 24, kitakwenda Zanzibar kucheza mechi za kirafiki dhidi ya wenyeji wao na baadaye watarejea jijini kujiandaa na mechi nyingine za kirafiki dhidi ya yosso wenzake kutoka Sudan, kati ya Novemba 8 na 10, mwaka huu.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinatarajia kuingia kambini ikifikapo Oktoba 29, mwaka huu na mechi mbili za kirafiki za kimataifa watakazocheza dhidi ya Sudan zitawasaidia kuwaimarisha wachezaji wake.

"Ninaamini mechi dhidi ya Sudan zitakuwa ni kipimo kizuri kwetu kujiandaa na michuano ya CECAFA, malengo yetu ni kufanya vizuri katika mashindano hayo na kuwa miongoni mwa timu mbili ambazo zitaenda kushiriki AFCON," alisema Julio.

Mbali na Super, wachezaji wengine aliowaita wanaocheza soka la kulipwa ni pamoja na Ally Msengi kutoka Stellenbosch ya Afrika Kusini, Novatus Dismas (Israel), Haji Suleiman (Porthmounth), Kelvin John (Leistercity Academy) na Nasir Saadun wa MFK Czech.

Kikosi kamili; Razaq Shekhmweri kutoka Mtibwa Sugar, Sheikh Abdallah (KMC), Emmanuel Charles, Ally Awilo, Pascal Gaudence, Laurent Alfred (Azam FC), David Kameta, Henry Hussein (Simba), Anderson Solomon (Dodoma FC), Shabani Kingazi (Mwadui), Jackson Nditi (Mtibwa), Omary Banda (Biashara United) na Lukonge Said wa (Fountain Gate).

Wengine ni Joseph Mkere (Mtibwa Sugar), Khlefinnin Salim, Ashraf Bashiri (Azam FC), Hassan Idd (KMC), Herbet Charles (Mbeya City), Feisal Hilal (Kagera Sugar),Frank Kahole (Mtibwa Sugar), Charles Masenga (Mwadui), Yussuf Shaban (Mbao), Adam Kihondo ( Yanga), Anuar Jabir (Dodoma FC), Michael Andrew (Simba), Mussa Gaddi (African Lyon) na Mohammed Yassin wa Lindi FC.

Michuano hiyo ya U-20 itakuwa ya kwanza kuandaliwa na CECAFA ikiwa chini ya Rais, Wallace Karia ambaye alichaguliwa kuliongoza baraza hilo kwenye uchaguzi uliofanyika jijini, Kampala nchini Uganda Desemba, mwaka jana.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot, Salmin Mohammed, akionyesha mfano wa zawadi ya hundi ya Sh. milioni 4.2 alizopata baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Washindi wa mechi 10 wamezawadiwa Sh. 729,534 huku Jackpot ya wiki hii ni Sh. milioni 248.7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Waamuzi, majaji wa ngumi kunolewa*

**Na Shufaa Lyimo**

WAAMUZI na majaji wanaosimamia mchezo wa ngumi hapa nchini wanatarajia kushiriki semina elekezi itakayofanyika Novemba 19, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Lugalo jijini, Dar es Salaam imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa semina hiyo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Super D Boxing, Rajabu Mhamila, alisema lengo la semina hiyo ni kuwajengea uwezo wa kufahamu sheria na kanuni za mchezo huo wasimamizi hao.

Mhamila alisema wanatarajia semina hiyo itashirikisha wadau 20 na wanawaomba wote watakaopata mwaliko kushiriki ili kufikia malengo.

"Tumeamua kufanya semina hii ili kuepusha malalamiko yanayotolewa na mashabiki wetu, katika siku za hivi karibuni kuna malalamiko ya kuwabeba mabondia, tunataka kulimaliza kwa kuwapa mafunzo yatakayosaidia kila mmoja ajue wajibu wake," alisema Mhamila maarufu Super D.

Alisema washiriki hao ndio watakaoteuliwa kuchezesha mapambano mbalimbali ya kufunga mwaka yatakayotangazwa hivi karibuni na wanaamini hayatakuwa na malalamiko.

Kiongozi huyo ameziomba kampuni na taasisi mbalimbali kujitokeza kudhamini mchezo wa ngumi ambao unasaidia kutangaza jina ya nchi kimataifa na unatoa ajira kwa vijana kama ilivyo michezo mingine.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 24, 2020
Nipashe




Arteta: Ozil atakiwa ajilaumu mwenyewe UKURASA 20



Winga wa Arsenal, Nicolas Pepe (kushoto), akijaribu kumtoka beki wa Rapid Vienna, Marcel Ritzmaier, katika mechi ya Kundi B ya Ligi ya Europa iliyochezwa jijini Vienna nchini Austria juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC yaweka rekodi mpya Bara

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE mabingwa watetezi, Simba imecheza kwa dakika 90 bila kupata bao kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara huku pia ikipoteza mechi ya kwanza msimu huu baada ya kucheza mechi tano.

Msimu uliopita ilipotwaa ubingwa, Simba ilipoteza mechi yake ya kwanza baada ya mechi sita ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC ya Shinyanga.

Si tu kwamba Simba ilipata mabao kwenye mechi hizo sita, lakini pia ilishinda zote, tofauti na msimu huu ambapo katika mechi hizo tano imeshinda mechi nne na kutoa sare moja.

Ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga, Rukwa juzi Simba ilichapwa bao 1-0 na Tanzania Prisons huku ikimaliza dakika 90 bila bao lolote baada ya kucheza mechi tano mfululizo ikifunga magoli.

"Ni sehemu ya matokeo ya mchezo. Naamini mwalimu ameona makosa na tutaenda kuyafanyia kazi ili mchezo ujao turudi vizuri zaidi." alisema nahodha msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' mara baada ya kumalizika kwa mechi hiyo.

Simba imefunga mabao 14 kwenye mechi tano zilizopita za ligi, ikianza kwa kuichapa Ihefu FC bao 1-0, na baada ya hapo ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar halafu ikaichapa Biashara United mabao 4-0 huku ilipokutana na Gwambina FC ilishinda mabao 3-0.

Katika mechi ya raundi ya tano, Simba itakayoiwakilisha Bara kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliifunga JKT Tanzania mabao 4-0, kabla ya kukwama kwenye mechi ya sita.

Katika msimamo wa ligi, Azam FC imeendelea kukaa kileleni ikiwa na pointi 21 ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 16 na mabingwa hao watetezi wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 13.

Kikosi cha Simba tayari kimesharejea Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa kuikabili Ruvu Shooting katika mechi itakayochezwa keshokutwa wenye Uwanja wa Uhuru.

# Kaze: Kikubwa ni pointi tatu

### ●●● Kocha huyo afunguka wachezaji Yanga sasa hawauogopi mpira, lakini...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wachezaji wake wameanza kuwa watulivu wanapokuwa na mpira tofauti na walivyokuwa zamani, lakini pia kwa sasa kikubwa ni kuona wanavuna pointi tatu katika kila mechi ya Ligi Kuu Bara watakayocheza.

**Tayari kikosi cha Yanga kimeshatua jijini, Mwanza kwa ajili ya mechi yao inayofuata dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.**

Akizungumza na gazeti hili, Kaze, alisema licha ya kukaa muda mfupi na timu hiyo, wachezaji wake wameanza kucheza kwa nafasi huku wakionekana hawana presha ya kupiga mbele.

Kaze, ambaye alianza na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania hapo juzi alisema amependa namna wachezaji wake walivyokuwa na akili ya kutulia zaidi wanapokuwa na mpira ingawa katika idara ya umaliziaji bado haijakuwa vizuri.

"Kipindi cha kwanza tumepoteza pasi nyingi, kipindi cha pili angalau tumecheza, lakini pia kipindi cha kwanza kumepoteza nafasi tatu au nne za kufunga, kipindi cha pili tulitembeza mpira, lakini hatukufanya hivyo muda wote, wachezaji wangu watazoea taratibu," alisema Kaze.

Mrundi huyo alisema kitu tofauti alichokiona kwenye mechi hiyo ni wachezaji wake kutokuwa na presha wanapokuwa na mpira na ndivyo alivyokuwa anataka.

"Mechi za nyuma nilivyokuwa nikiona walikuwa wanapata presha wanapiga mbele, lakini kwenye mechi hii wamekuwa watulivu," Kaze alisisitiza.

Kocha huyo alisema bado anahitaji muda wa kukijenga kikosi hicho na kueleza siku tano alizoongoza mazoezi hazitoshi kubadilisha kiwango cha wachezaji wake ingawa wamemfurahisha kwa walichomwonyesha.

"Kipindi cha pili timu ilicheza vizuri, licha ya kupoteza nafasi, ila malengo yangu ya kwanza ni kupata pointi tatu, pamoja na wachezaji kufanya nusu ya kile ambacho nimewaelekeza katika mazoezi, Fei Toto (Feisal Salum), peke yake alipoteza nafasi mbili," Kaze alisema.

Kuhusiana na suala la kumiliki mpira, Kaze alisema wachezaji wake hawakufanya vile alivyotaka ingawa anaamini siku zinavyozidi kwenda watafanya anachokihitaji na kupata matokeo mazuri zaidi.

"Ni ngumu kwa siku tano kukaa na timu na wachezaji kufanya kile ulichowaelekeza Ila amefurahi kuona kila mchezaji anajituma na kuonyesha kila mmoja anataka kucheza," alisema Kaze.

Alieleza tayari amewapa washambuliaji wake programu maalumu za mazoezi ili kuhakikisha anapunguza 'ukame wa mabao' na kuitaja safu ya kiungo pia inashindwa kupa pasi za kutosha mastraika wao.

"Nimeanza kuiboresha safu hiyo ya ushambuliaji kwa kuhakikisha natengeneza muunganiko mzuri wa viungo na washambuliaji ambao kabla ya kuja kwangu haukuwepo, tusiwe na haraka, mambo mazuri yataonekana huko mbele," alisema Kaze.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga inaongozwa na Michael Sarpong, Yacouba Songne, Waziri Junior na Tuisila Kisinda, na hadi sasa imefanikiwa kufunga mabao nane pekee.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042



9 770856 541002 >